Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 74 No. 180 | JAMAD I/JAMAD II 1435 AH | APRIL 2014 | SHAHADAT 1393 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Na katika watu wako wanaoshika washirika kinyume cha Mwenyezi Mungu, wanawapenda kama kumpenda Mwenyezi Mungu. Lakini walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana; ...
(*Al- Baqara*) (2:166).

Khalifatul Masih awakumbusha Waahmadiyya

Ukhalifa ndio nguvu ya umoja wetu

Maombi ndio silaha yetu

Msaada mkubwa wa Mwenyezi Mungu ambao umeiunganisha jamaat Ahmadiyya kuwa kitu kimoja na ambao umekuwa ukiendelea tangu kufariki kwa Masihi Aliyeahidiwa (as) ni taasisi ya Khilafat. Miaka 106 iliyopita ya historia ya Jamaat inashuhudia ukweli kwamba baada ya kifo cha Masihi Aliyeahidiwa a.s., kama alivyosema katika kijitabu chake Alwasiyyat wanajumuiya wameikubali Khilafat kwa utii kamili. Kila Muahmadiyya duniani kote bila kujali kabila au taifa lake anatambua vizuri sana kwamba kushikamana na Khilafat katika misingi ya unabii ambao ulikuwa uanze baada ya kudhihiri kwa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) ndio wajibu wake mkubwa kabisa.

Huzur alisema hapa hakujumuisha wale waliojitenga katika miaka ya mwanzo ambao sasa hawajulikani, bali anamaanisha kundi la wanajumuiya walio wengi ambao wanaelewa ahadi ya Masihi Aliyeahidiwa (a.s) na wanao uelewa kwamba katika kushikamana na ukhalifa ndimo ulimo umoja wao, maendeleo yao, na kutokana nao hupatikana nguvu za kujibu mashambulizi ya maadui wa Ahmadiyyat, na Islam. Hii ni kwa sababu msaada na ulinzi wa Mwenyezi Mungu sasa unaambatana na ukhalifa wa awamu ya pili ya Islam.

Hata hivyo inabidi ieleweke kwamba mtu kutamka imani yakwe kwa mdomo tu, hakuvutii rehema ya Mungu.

Ayat e Istikhlaf (Aya ya 56 sura Al-Nuur) inaahidi ukhalifa kwa waaminio wa kweli na inatoa habari njema ya kubadilisha hofu yao kwa amani na inaahidi kuwastawisha. Hii bila shaka ni ahadi kwa wale wanaosimamisha sala, wanaomuabudu Mwenyezi Mungu na wanaojitoa muhanga kusimamisha

Endelea uk. 3

Ij'timaa ya Khuddam yaleta Mapinduzi Mapya

- *Atfal waadhimisha Ijtimaa yao ya Pili*
- *Khuddam kutoka Kenya na Uganda washiriki kwa pamoja kwa mara ya kwanza.*
- *Waumini wa madhehebu mengine wafunga safari kutoka Kenya kushiriki Ijtmaa*

Na Mwandishi wetu

Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu Mtukufu, Tanzimu ya Khuddamul na Atfalul Ahmadiyya imeadhimisha Ijitmaa yake ya 25 siku chache zilizopita katika viwanja vya Jalsa Gaal, eneo la Kitonga jijini Dar Es Salaam.

Ijitmaa hiyo iliyochukua takribani siku tatu kuanzia Ijumaa ya tarehe 20, 21 na 22 mwezi Juni mwaka huu, iliwakutanisha vijana wa Kiahmadiyya (Khuddamul na Atfal) wapatao mia nne na sitini kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani pamoja na wengine kutoka nchi jirani za Kenya na Uganda.

Katika siku hizo zote tatu, vijana walipata fursa ya kujumuika na kushirikiana pamoja katika mambo mbalimbali ya kimwili na kiroho ikiwemo kushindana katika mambo ya kielimu na michezo. Pia, vijana waliweza kupata nafasi kubadilishana mawazo ya kielimu na kidini, kula na kusali pamoja kwa nyakati zote za sala, jambo ambalo ni muhimu katika kukuza umoja, ushirikiano na upendo baina yao.



Amir na Mbashiri Mkuu Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry kwenye Ijtimaa ya Khuddam na Atfal, kushoto Sadr Khuddam Uganda - Dr. Haroun Mubiru, kulia Dr. Saleh Kitabu Pazi Sadr Khuddam Tanzania

Ujumbe wa mwaka huu katika Ijitmaa ulikuwa ni Aya ya 64 ya suratul Al Furqan isemayo:

Na watumishi wa Rahmani ni wale wanaotembea ardhini kwa unyenyekevu, na wajinga wakisema nao husema: Amani; Huku Amani na unyenyekevu vikiwa ndio maudhui ya ujumbe huo.

Ufunguzi

Mara baada ya sala ya Ijumaa ya tarehe 20 na kufuatiwa na hotuba ya Huzur, Ijtmaa ilifunguliwa rasmi na Sadri Sahib, Dkt. Swaleh Kitabu Pazi mara baada ya kuwatambulisha wageni mbalimbali walikuja kushiriki katika Ijtmaa hiyo wakiwamo Masadr wa nchi za Uganda na Kenya sambamba na wajumbe kadhaa waliofuatana nao wakiwemo Viongozi wa Majlis za nchi hizo mbili. Wa kwanza kutambulishwa alikuwa ni Sadri Sahib wa nchi ya Kenya, Dkt ……. Ambaye aliwakumbusha Khuddam umuhimu wa kushindana katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa kunukuu aya ya Qur'an Tukufu isemayo:

……..

Akafuatiwa na Sadri wa Uganda Ndugu, Mubiru ambaye hii ilikuwa ni Ijtimaa yake ya Pili kushiriki mbali na ile ya mwaka 2011. Akitoa salamu zake za Ijtmaa kwa Khuddam, Sadr Sahib wa Uganda aliwataka khuddam kujitahidi katika kufanya matendo yaliyo mazuri na kutia bidii katika kumuelekea Mwenyezi Mungu. Alisema kuwa, vijana ndio watakaoifanya jumuiya ipate maendeleo na ikiwa vijana hawatakuwa na nia ya dhati ya

Endelea uk. 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

MAPINDUZIYAKWELI

Mwaka mmoja kabla ya kuanzishwa mapinduzi ya kimwili yalianza mapinduzi ya kiroho. Mwaka 1953 Jumuiyya ya Ahmadiyya ilitoa tafsiri ya kwanza ya Qur'an Tukufu kwa lugha ya Kiswahili na mwaka uliofuata 1954 kilizaliwa chama cha Tanganyika African National Union (TANU) kilicholeta ukombozi wa nchi hii.

Siku za mwanzo za mapambano yetu ya uhuru zilitawaliwa sana na athari iliyotokana na tafsiri ya Qur'an Tukufu. Wana TANU wa mwanzo hawakuanza vikao vyao bila maombi. Maneno; "Nitasema kweli daima fitina kwangu ni mwiko" yalitawala enzi hizo. Usafi wa khulka uliheshimika. Rushwa ilihesabiwa kuwa ni adui wa haki. Ufahari wa kujitutumua na kujiona vilikuwa baidi na wana TANU. Kujitolea ilikuwa ni sera iliyoshika kasi sana. Akina mama wauza vitumbua walitoa thumni zao na ndio hao waliompa mapokezi makubwa 'Baba kabwera' aliporudi kutoka umoja wa mataifa. Zilikuwa ni enzi nzuri za matumaini na kujiamini. Zilikuwa ni enzi za kujiheshimu na kukataa. Ilikuwa ni fahari kuwa mwana wa taifa hili. Wale wakoloni waliowahi kutawala maarufu kwa 'mkono wa damu' tuliwapa saa 24 kufunga virago vyao kwa sababu walidiriki kuingilia mambo yetu ya ndani. Tofauti za kipato hazikuwa kubwa na matajiri hawakuwakoga maskini. Kwa hakika walijitolea zaidi katika maendeleo ya jamii yetu. Watu wasiojiweza kifedha ndio waliojaa bungeni. Sifa ilikuwa moja uwezo na nia ya kuwatumikia wakulima na wafanyakazi.

Tizama mageuzi tuliyo nayo sasa. Kitu kinachoabudiwa (Mungu Apishe mbali) ni fedha. Huwezi kutia mguu wako Bungeni iwapo wewe ni maskini. Mahakamani usahau kabisa haki yako ikiwa una mkono wa birika. Hospitali utakata roho kama hukubeba chochote mfukoni. Shule zimebaki kwa wale ambao sasa

wanakula kwa niaba yetu. Ukarimu mkubwa wa Mtanzania kwa hivi sasa ukipata ajali huruma yao ya kwanza ni kukagua ulicho nacho mfukoni. Je unayo mafao? Utu wako utakuja baadae. Hapo ndipo tulipofika. Hapo ndipo tulipo. Kwa maneno ya Mwalimu Nyerere "mbele moto, nyuma moto". Swala la kujiuliza kwa hivi sasa kwa wale wote wenye uchungu na nchi hii, 'tufanye nini' tufanye nini kupunguza matusi bungeni, tufanye nini watoto wetu wapate elimu wanayostahili mashuleni. Tufanye nini mvua inaponyesha isituaibishe kuonyesha kwamba hatuna barabara kabisa. Tufanye nini kujenga daraja ambazo zinaweza kudumu kama ile ya Sarenda Bridge.

Tufanye nini ili kurejesha heshima tuliyokuwa nayo tulipopata uhuru? Sisi tunaamini kabisa kwambakila ugonjwa una dawa yake. Tunadhani kama tulivyokuwa mwanzoni inatubidi tuwe hivyo kwa hivi sasa. Hakuna njia isipokuwa kuzaliwa mara ya pili. Kusafisha nafsi zetu, kurejea kwa Mola wetu. Kurejea katika katiba ambayo itaweza kuisadia nchi hii kwenda m bele. Tunadhani kwa msaada mkubwa wa Mwenyezi Mungu tunazo katiba zinazotufaa sana ambazo zingeweza kumaliza matatizo yetu tuliyo nayo. Je kuna katiba iliyo bora kuliko Qur'an Tukufu? Je ndugu zetu Wakristo wana katiba bora kuliko Biblia? Kama sote tunaweza kuviheshimu vitabu vyetu hivi, tukafuata mafundisho yake kwa vitendo na sio maneno haja ya kuwa na katiba itaondoka. La msingi sio kuwa na katiba, la m singi ni kuwa na nafsi zilizosafishwa kwa khofu ya Aliyetuumba. Hiyo ndiyo katiba inayoweza kuzaa katiba zote. Na ndiyo maana mahangaiko yetu yote ya kutafuta katiba yamekosea. Kwa sababu katiba tayari tunayo. Ni kuzifuata katiba hizo ambazo zote zinazungumzia juu ya mapenzi, uelewano, kuheshimana, kusaidiana na kujiletea maendeleo.

Tunadhani ya kwamba ulafi wetu wa mali unachangia kwa kiwango kikubwa maanguko yetu. Lakini tujiulize wale waliokusanya mali hizo bila kuonesha dalili yoyote ya kuwasimanga wako wapi hivi leo na mali zao? Viongozi maarufu wa Afrika wako wapi? Na fedha hizo ziliwasaidia nini? Ukumbusho huo utatusaidia kurejea katika misingi madhubuti ambayo tuna uhakika ya kwamba italeta mageuzi makubwa. Dawa ya tatizo letu ni kumtii Mwenyezi Mungu na kuendeleza mapinduzi ya kiroho. Hiyo ndiyo nusura ya taifa letu.

Hotuba ya Bw. Ode - Amir wa Falastin

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

Hamdu zote za wale wanaohimidi zinamhusu Mwenyezi Mungu na baraka na rehema ziwe juu ya Hadhrat Muhammad Mteule saw, Muhuri wa Manabii na Mbora wa Mitume wote.

Mheshimiwa mwenyekiti na wasikilizaji wapendwa, Jibrili alaihi salaam alipomleta Hadhrat Mahdi Maahud as katika kijiji cha Qadiyan, basi katika milima ya hapa habari zake zilienea kote. Ardhi hii ibarikiwe ambamo ndani yake Mahdi alikuja akiwa mwenye kufanya jihadi, ambaye mkononi mwake ulikuwa upanga kali wa kutetea haki.

Sisi watumishi wa Imamu,tumetokea nchi moja ya Arabu Palestina ambayo ni maskani wa mitume na kufika Qadiyan ili tuitimize haki ya amana ile iliyokalifishwa juu yetu na Mtume saw,yaani kuifikisha salamu ya Mtume Mtukufu saw kwa Mahdi wake mpendwa na Masihi aliyeahidiwa as.Hivyo sisi kwa sauti ya juu twakupatia zawadi ya Assalamo Alaikum warahmatullah wabarakatohu itokayo kwa Mtukufu Mtume saw na vilevile kusema Assalamo Alaikum warahmatullah wabarakatohu kwa wakazi wa Qadiyan.

Ndugu zanguni,Syedna Ahmad as alikuwa akiwapenda sana Waarabu na kuipenda sana ardhi yao,hivyo anasema kwamba Mwenyezi Mungu Amenipatia bishara ihusuyo Waarabu na kunifunulia ya kuwa mimi niwasaidie na kuwaongoza kwenye njia iliyonyoka na kuzirekebisha hali zao.Na kuhusiana na hayo Mungu Akijaalia mtanikuta mwenye kushinda.

Seyidna Ahmad as aliwajali sana Waarabu kwa moyo wake wote na kuvituma vitabu vyake katika nchi zao,ijapokuwa watumishi wa sultani walikuwa wakivichoma vitabu vile.Huzur as anasema katika kitabu chake kiitwacho Hamama tul Bushra kwamba mimi napenda kuwatumieni vitabu hivi lakini nimesikia ya kuwa watumishi wa sultani kwa kuwa na dhana mbaya baada ya kuvisoma wanavichana vitabu. Basi enyi wapendwa wangu niambieni,kwa namna gani vitabu hivi vinaweza kuwafikia nyinyi,nami pia kuhusiana na hilo najitahidi na kushauriana na watu wenye uzoefu.

Leo sisi tunasema kwamba naam,ewe kiongozi wetu,mwito wako umefika tayari katika nchi za Arabu,kwa nyumba za Waarabu,mpaka masikioni mwao kwa kupitia MTA.MTA ya tatu ambayo mpendwa wetu Khalifa tul Masihi wa Tano aliitamani tu,basi Mwenyezi Mungu Aliitimiza tamanio lake kwa ufanisi mkubwa.

Safari moja Khalifa Mtukufu alisema ya kwamba nyinyi kwa kuitafuta satalaiti yoyote ya Arabu,kwa nini hamrushi vipindi vya MTA juu yake?Mimi kwa sababu ya uelewa wangu mdogo nilifikiri ya kwamba labda Huzur alikuwa hajui hali ya huko ikoje kwani haikuwezekana kabisa ya kuwa Waarabu wangetupatia ruhusa ya kurusha MTA,lakini linalopangwa na Mungu bila shaka kutimia ni wajibu. Mwenyezi Mungu Alimfunulia Masihi Aliyeahidiwa as "INNI MAAKA YA MASRUUR"yaani kwa hakika mimi nipo pamoja nawe ewe Masruur,hivyo kwa kusema kwa Huzur tu,vikwazo vyote vilitoweka na katika muda mfupi tulifunga mkataba na satalaiti Nile ya Misri na kwa fadhila ya Allah MTA Alarabia ilianza kurushwa juu yake. Huzur alituelekeza upande huu ya kuwa sisi tuzijibu tuhuma ziletwazo na chaneli za Arabu za kikristo dhidi ya Islam ambazo zilikuwa zikianzisha harakati za kuueneza ukristo humo,hivyo tulianza kutoa majibu ya propaganda iliyofanywa nao dhidi ya Islam na dhidi ya Mtukufu Mtume Muhammad saw.Kwa sababu ya maombi ya Khalifa Mtukufu"Mwenyezi Mungu Awasaidie"Mungu Awanusuru"uchawi wa mchawi ulimrudia kwake,na padre mkuu wa Misri alikiri juu ya MTA ya kuwa nyinyi mmekuwa usumbufu mkubwa kwa ajili ya kanisa la kikristo,hivyo watu wengi walioingia kwenye Ukristo,kwa fadhila ya Allah na kwa maombi ya Huzur wakarudi tena katika Islam.Hivyo kanisa la Qibti,kwa lengo la kusitisha huduma ya MTA lilipeleka malalamiko mahakamani lakini hawakufanikiwa kisha waliomba msaada kutoka rais wa Misri,watu hao walisaidiwa na mawahabi vilevile,hivyo tarehe 28 Januari 2008 MTA Alarabia ilifungwa wakati ambapo Baraka na salamu ilikuwa ikitumwa juu ya Mtume saw.

Mpinzani alielewa hivi ya kwamba wamekomesha sauti ya Masihi wa Muhammadi na wakafurahi sana juu ya hilo ,lakini furaha yao hii haikubaki kwa muda mrefu,mbingu ilighadhibika juu ya tendo lao.Huzur alisema hapo (FADAMDAMA ALAIHIM RABBUHUM BIDHAMBIHIM FASAWWAHA)yaani kwa hiyo Mola wao Aliwaangamiza kwa sababu ya dhambi zao na Akawafukia ardhini na kuisawazisha.Hivyo baada ya kupita siku chache tu,tangu MTA ifungwe waya tatu za kugawa huduma ya intaneti katika Misri zilifungwa zenyewe na mpaka leo haikujulikana ya kwamba zilifungwaje?Zaidi ya hayo,siku ambapo walifunga matangazo ya MTA,baada ya kupita miaka mitatu katika siku ileile wananchi wa Misri walianza kuandama dhidi ya rais yule yule wa Misri,hivyo angalieni kwa namna gani na kwa shani gani ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kuwaangamiza ilitimia barabara na jambo alilosema Hadhrat Amir ul Muuminiin lilithibiti kwa shani gani?

Huyu ndiye Mungu wetu Aliye hai Ambaye Alimwambia Syedna Ahmad as kwamba INNI MAAKA YA MASRUUR basi maadamu tutaendelea kuungana na Ukhalifa na Mungu Yupo pamoja nasi,nguvu yoyote ya dunia haiwezi kuleta kikwazo katika njia yetu,kutokana na kujiunga na Ukhalifa,Mungu Yupo pamoja nasi,hivyo baada ya kufungwa kwa MTA ALarabia satalaiti ya Misri Nile iliangamia na Misri na nchi nyingi za Arabu zililazimika kupeleka matangazo yao kwenye satalaiti nyingine, hata hivyo kulikuwa na sehemu moja juu yake iliyokuwa ikinunuliwa na kampuni moja ya Ulaya,hivyo kuanzia muda ule mpaka leo sisi tunaendelea kurusha matangazo yetu juu ya satalaiti ile ile.Alhamdulillah

Kwa fadhila ya Allah watu wengi kutoka nchi mbalimbali za Uarabuni, baada ya kufanya baiat wanaingia katika Jumuiya na kwa fadhila ya Mwenyezi Mungu ufunuo wa Syedna Ahmad as usemao,Mwenyezi Mungu Amenipatia habari njema ihusuyo Waarabu na kunifunulia kuwa mimi niwasaidie na kuwaongoza kwenye njia iliyonyoka na kurekebisha hali zao na nyinyi kuhusiana na hilo mtanikuta, Mungu Akijaalia mwenye kushinda, unaendelea

Endelea uk. 4

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Ukhalifa ndio nguvu ya umoja wetu

Kutoka uk. 1

Tawheed. Wapo wengi wanaosema 'La ilaha ila Llah' (hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah) lakini kwa hakika wanaoelewa 'La ilaha ila Llah ni wale tu ambao humwelekea Mungu tu katika hali zote na ambao hawamwelekei mwingine yeyote isipokuwa Mungu. Kila siku ya Ukhalifa ambayo tunaidhimisha inabidi itupeleke kwenye ibada ya Mungu, Sala, kusimama imara katika Tawheed na vile vile katika kupima kiwango chetu cha kueneza tawheed (umoja wa Mungu). Kama viwango vyetu katika uwanja huu haviongezeki, basi kufanya maadhimisho, kutoa hotuba, mihadhara ya kisomi na sherehe zinginezo hakuna maana yoyote. Kinachotakiwa ni kuelewa kiini cha yote hayo. Tutaelewa ukweli wa umoja wa Mungu ikiwa tutaelekea kwenye maombi na tutakapofanywa wapokeaji wa rehema ya Mungu ambayo iliahidiwa kwa Masihi Aliyeahidiwa (a.s).

Mwenyezi Mungu anazielekeza fikra zetu kwenye maombi na taqwa yake ili tubaki katika maungano na ukhalifa, tufikiwe na rehema ya Mungu, tuondolewe tabu zetu na kupata amani ya moyo na maombi na taqwa kwa hakika ndio silaha zetu za kweli ambazo tunaweza kuzitegemea wakati wote. Njia na mbinu za kidunia hazileti mafanikio. Tunajifunza kwamba katika masimulizi ya historia za Manabii wa Mungu mafanikio yalikuja kwa maombi tu, hususan katika historia ya Islam na kipekee katika wakati wa Mtume Mtukufu s.a.w. na Khilafat e Rashdeen (Makhalifa waongofu) ushindi ulikuja kwa njia ya maombi na sio kwa njia za kidunia. Yapaswa ikumbukwe hata hivyo kwamba pamoja na ahadi zote za Mungu, muhanga wa maisha uliotolewa na viwango vya taqwa daima vilikuwa vya juu.

Huzur alitaja kwa mapitio kwamba Ijumaa iliyopita alieleza kuhusu Muahmadiyya ambaye rafiki yake wa Kishia alimwambia kwamba Waahmadiyya hawayakabili mambo kama ipasavyo na Huzoor akasema kwamba yaelekea yule Muahmadiyya pia alikuwa na maoni hayo hayo. Ingawa Huzur hakutaja jina lolote yaelekea yule mtu alijielewa na kumwandikia Huzoor akisema ya kwamba yale yalikuwa ni maoni ya rafiki yake Mshia na kwamba yeye hakuwa na maoni kama hayo. Huzoor akasema kwamba anapata habari kutoka vyanzo mbalimbali kwamba wapo watu wenye maoni kama hayo. Yatupasa tukumbuke kwamba baraka zote ziko katika maombi, kama Mwenyezi Mungu alivyosema: Basi usali kwa Mola wako na utoe dhabihu. (108:3).

Ni ibada ya Mungu na dhabihu ndiko kunakotufanya wapataji wa baraka za Mungu.

Hakuna shaka kwamba imo katika maumbile ya binadamu kuhamanika pale majaribu na mashaka yanapokuwa ya muda mrefu. Kama ilivyotajwa katika Ijumaa iliyopita katika hali kama hizo waumini wa kweli huita kwa sauti yenye hangaiko isemayo: …

Msaada wa Mwenyezi Mungu utakuja lini? … (2:215).

Wanasema hivyo sio kwa kukata tamaa bali kuvutia huruma ya Mwenyezi Mungu ; wanafanya hivyo kwa kujitoa kikamilifu na kujitupa kwa Mungu, wakiziinua sala zao kwenye kiwango cha juu kabisa na wakiwa katika hali ya juu kabisa ya kujitoa muhanga. Na ndipo, kwa majibu, inakuja sauti .. "Bila shaka msaada wa Mwenyezi Mungu uko karibu" (2:215).

Mwenyezi Mungu Alimpa ufunuo huu Masihi Aliyeahidiwa (a.s) katika matukio mbalimbali na pia akaonyesha jambo hili kwa matendo na sisi pia tu mashuhuda wa jambo hili na Inshallah tutaendelea kuwa mashuhuda wa jambo hili. Msaada wa Mungu huja katika nyanja maalum na bila shaka kuna hatima ya ushindi mwanana wa msaada wa Mungu na ulinzi ambao tutaushuhudia!

Adui anapanga hila za hatari. Kwa mtazamo wa kidunia hali katika nchi za kiislam hususan Pakistan ni ya kutisha sana. Hata hivyo Mwenyezi Mungu anao uwezo juu ya kila kitu na Yu Mbora wa wapangaji mipango na atazihafifisha njama za adui kuwa mavumbi! Tunahitaji kugeukia sala na Istighfar, kuondoa wasi wasi wetu na ili tuweze kutunza ushindi wetu.

Mwenyezi Mungu anasema:

Basi Mtukuze Mola wako kwa sifa njema, na umwombe ghofira; hakika Yeye ndiye Apokeaye sana toba. (110:4).

Wote twahitaji kulielewa somo hili na tunahitaji kuzikweza sala zetu kufikia vilele vya juu kabisa. Huzoor alisema kwamba aliwahi kusema kabla kwamba tunao uelewa wa hali ya juu wa moyo wa kujitolea lakini twahitaji kuelewa hakika ya Sala. Ili tuweze kufaidi matunda ya kujitolea kwetu, tunahitaji sana kupandisha ubora wa sala zetu na twahitaji sana kupandisha hali ile ndani yetu ambayo Mungu anaitaka.

Mwenyezi Mungu anasema:

Au ni nai Anayemjibu aliyedhikika amwombapo na kuondoa dhiki, na kuwafanyeni waandamizi duniani? Je, yuko mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ni kidogo mnayoyakumbuka.(27:63)

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) aliandika:

Kumbukeni Mwenyezi Mungu si mwenye kujali chochote na isipokuwa kwa maombi yanayofanywa kwa wingi na kwa vilio; Yeye hajali. (Kujali kwa Mwenyezi Mungu sio kama kwa binadamu - hii iaonyesha utukufu wake, kutokuhitaji chochote, wala kuhofu chochote) Mtu ambaye mke wake au mtoto anaumwa au pale mtu anapokabiliwa na huzuni kuu, anakuwa amefadhaika sana. Bila maombi kuwa na ukweli wa moyo na ya dhati kabisa na yaliyofanywa katika hali ya fadhaiko yanakosa athari na yanakosa maana. Ni lazima kwamba maombi yafanywe kwa moyo wenye taabiko ili yaweze kupokelewa, kama isemavyo:

Au ni nai Anayemjibu aliyedhikika amwombapo na kuondoa dhiki,… (27:63).

(Tafseer: Promised Messiah vol. 111, p 574).

Tunahitaji kuweka mkazo kwenye maombi na taqwa zaidi kuliko wakati wowote na tunahitaji kufanya maombi hayo kwa vilio na kwikwi za moyoni na tunahitaji kuvutia huruma ya Mungu.

Halafu Huzoor akazielekeza fikra zetu kwenye baadhi ya maombi ambayo kwanza yalihimizwa na Khalifatul Masih III (r.h.) wakati wa sherehe za karne ya Jamaat. .. Na yeye Khalifa Mtukufu akazikumbusha tena wakati wa sherehe za karne ya Ukhalifa.

Maombi haya yapaswa yasisahauliwe wala kupunguzwa, kinyume chake yanatakiwa yawe sehemu ya maisha yetu ya kila siku. Zaidi ya hapo tunahitaji kuyaweka kwenye sala zetu. Maombi haya yanasomwa mara kwa mara kwenye MTA lakini Huzur aliyataja pia kwa kukumbusha.

(1) Kwanza kabisa ni sura Al Faatehah, inapaswa isomwe kwa wingi.

(2) Darud (sala ya Mtume) yapaswa pia kusomwa kwa wingi.

(3) Kisha kuna maombi yaliyofunuliwa kwa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) nayo yasomwe kwa wingi.

"***Subhaanallah wabihamdihii, Sunhaanallahul adhiim, Allahummaswally 'alaa Muhammad wa'alaa Aali Muhammad.***"

Hadhrat Abu Huraia r.a. anasimulia kwamba Mtume Mtukufu s.a.w. alisema: Kuna kauli mbili ambazo ni nyepesi kwenye ulimi wa mtamkaji lakini zina uzito mkubwa katika mizani na zinapendwa sana na Mwenyezi Mungu Mwenye Rehema. Nazo ni "***Subhaanallah wabihamdihii, Sunhaanallahul adhiim.***"

Tafsiri: Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu na sifa Zake, Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu mwenye adhama. Ee Mwenyezi Mungu Msalie Muhammad na ahali (watu) wa Muhammad

Huzur kasema kwa kuwa sentesi hizi zinapendwa na Mungu Mrehemevu, twahitaji kuzisoma ili kuvutia huruma yake.

(4) Kisha kuna maombi:

"***Rabbanaa laa tuzigh quluubana ba'ada idh hadaitanaa wahab lanaa minladunka Rahmatan Innaka antal Wahhaab***"

Mola wetu, Usiipotoshe mioyo yetu baada ya kutuongoza, na Utupe rehema kutoka Kwako, hakika Wewe ndiwe Mpaji Mkuu. (3:9).

Hazrat Nawab Begum sahiba r.a. alipata ndoto baada ya kufariki Masihi Aliyeahidiwa (a.s) ambamo alimshauri kuomba hivyo kwa wingi. Aliposimulia ndoto yake kwa Khalifatul Masih I r.a. alisema yeye mwenyewe (Khalifa) hataacha kufanya maombi hayo kwa wingi. Alisema kwa wakati maombi hayo yanaombea nguvu ya imani, yalikuwa pia yanaombea kubaki katika maungano na Ukhalifa.

(5) Maombi mengine ambayo twahitaji kutilia mkazo ni:

"***Rabbanā Afrigh 'alaynā swabra wathabbit aqdāmanā wanswurnā 'alal qawmil kāfiriin.***"

Mola wetu, tumiminie subira, na Utuimarishe miguu yetu, na Utusaidie juu ya watu makafiri. (2:251)

(6) Kuna hadithi inaeleza kwamba wakati Mtume Mtukufu s.a.w. alipokuwa akihisi hatari kutoka kwa kundi la watu, alikuwa akisoma maombi haya.

Allahumma Innaa Naj'aluka fii nuhuurihim wana'udhubika min shuruurihim

Ee Mwenyezi Mungu tunakuweka wewe mbele ya vifua vyao (yaani uwe kinga yetu dhidi yao) na tunajikinga kwako na shari zao.

Inapasa vile vile kuendelea kufanya Istighfar kwa wingi kwa kutamka:

(7) ***Astaghfirullahi Rabby min kulli dhanbiy waatuubu Ilayhi.***

Ninamuomba Allah Mola wangu, msamaha wa dhambi zangu zote na ninatubu / naelekea Kwake.

(8) Muda kidogo uliopita Huzur alihimiza kufanyika kwa wingi maombi haya kwa mujibu wa ndoto yake:

Rabbi Kullu shayin Khaadimuka rabbi Fahfadhny, wanswurny warhamny.

"Ewe Mola, kila kitu kinakutumikia wewe, Ee Mola, utulinde, utusaidie na utuhurumie"

(9) Maombi yaliyoelekezwa katika sala ya Ijumaa iliyopita yanatakiwa yaingizwe pia katika maombi ya mara kwa mara.

"***Rabbanā ghfirlanā dhunuubana wasiarāfana fii amrinā wathabbit aqdāmanā wanswurnā 'alal qawmil kāfiriin.***"

Mola wetu, Tughofirie madhambi yetu na kupita kwetu kiasi katika mambo yetu na uiimarishe miguu yetu na Utusaidie juu ya watu makafiri. (3:148).

Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alisema: Nilikuwa naomba kwa ajili ya wanajumuiya wa Jamaat yangu na kisha kwa ajili ya Qadian wakati ufunuo uliponijia: "Wamejitenga na utamaduni wa maisha! Na wasage tikitiki! Masihi Aliyeahidiwa (a.s) akasema: Nilishangaa kwa nini tendo la kusagwa tikitiki limenasibishwa na mimi. Kisha akaangalia maombi yaliyobandikwa kwenye ukuta wa chumba cha kusalia kama ifuatavyo:

(10) ***Yaa Rabbi fasma'a du'aaii wamazziq a'daaii wa'daaika, waan'jiz wa'daka wanswur 'abdaka, waarinaa ayyaamaka washahhir lanaa husaamaka walaa tadhar minal kaafiriina shariira.***

" Ee Mola, Sikia maombi yangu na uwasage maadui zako na maadui zangu na utimize ahadi yako na umsaidie mtumishi wako na utuonyeshe siku zako na ulinoe kwa ajili yetu panga lako na usimbakishe hata mmoja miongoni mwa makafiri mfanya vitimbi.

(Tadhkira, p. 664, 2009 edition).

(***NB: Dua hizi zote zimechapishwa kwa Kiarabu kwenye uk.*** 5).

Kisha Huzur alisema atamkumbuka mpendwa, mwaminifu, mtiifu, na mtu mwenye manufaa sana ambaye pia alikuwa na sifa nyingine nyingi. Huyu alikuwa ni Dr. Mehdi Ali Qamar, mtoto wa Chaudhry Farzand Ali Sahib. Aliuwawa Rabwah tarehe 26

Endelea uk. 4

Ukhalifa ndio nguvu ya umoja wetu

Kutoka uk. 3

Mei 2014. Alikuwa anakwenda kutembelea Bahshit Makbara Rabwah pamoja na mkewe, mtoto mmoja na ndugu mmoja baada ya alfajiri ndipo watu wawili wasiojulikana walikuja na pikipiki na kumpiga risasi. Dr. Mehdi Ali alikuwa daktari bingwa wa moyo (cardiologist) kutoka USA ambaye alikuwa anatembelea Rabwah pamoja na mkewe na watoto wawili kwa mpango wa waqfe Arzi (kujitolea kufanya kazi kwa muda mfupi) katika taasisi ya moyo ya Tahir (Tahir heart Institute).Alikuwa akikaa katika taasisi hiyo na siku ya tukio alikuwa anatembelea makaburi baada ya sala ya Alfajiri. Alipokaribia geti la makaburi watu wawili walitokea kwenye pikipiki na kumpiga risasi na walikimbia katika barabra kuu. Dr. Mehdi alipigwa risasi mara 11 na alifariki hapohapo. *Ina Lilahi wainaa ilahi rajiouun.*

Huzur alizungumzia mengi juu ya sifa za daktari huyu, kujitolea kwake, tabia zake njema, mafungamano yake na ukhalifa, mapenzi yake ya tabligh, huruma zake kwa wanadamu na hasa wagonjwa wake n.k. n.k

Pia Huzur alinukuu magazeti na vyombo kadhaa vya habari vilivyolielezea tukio hilo kwa masikitiko na mshit-uko mkubwa.

Mwishoni Huzur akasema:

Huyu Shahidi mpendwa amemwaga damu yake katika udongo wa Rabwah na kuelekeza fikra zetu kwenye maombi na upangaji mipango. Kwa hiyo kuna haja kubwa ya kuzingatia. Waahamdiyya duniani kote wanatakiwa kuwaombea Waahamdiyya wa Pakistan kwa sababu sasa wanaishi katika mazingira yasiyovumilika kabisa na hali inaendelea kuwa mbaya zaidi. Mwenyezi Mungu atuwezeshe kufanya hivyo.

Nchi nzima imekuwa ni hadithi ya ukatili na ukandamizaji, siku chache zilizopita mwanamke mmoja alipigwa mawe mpaka akafa nje ya Mahakama kuu. Mauaji na uvunjaji wa amani hutokea huko kila siku na hatuwezi kusema kwamba ni dhidi ya Waahamdiyya pekee. Wakati mauaji haya yalipotokea, ukandamizaji huu ulipotokea, bila shaka maafisa wa polisi walikuwepo na itakuw ayalitokea mbele yao.

Ukandamizaji huu huko Pakistan unafanywa kwa jina la Mungu na Mtume wake. Katika jina la Mjumbe ambaye alikuwa ni mhisani kwa wanadamu, aliyekuwa ni rehema kwa walimwengu. Nyoyo zetu zinavuja damu kwa ajili ya jambo hili. Kama ni lazima wafanye ukandamizaji angalau wasifanye kwa jina la Mungu na Mtume wake. Wasifanye mateso kw aajina la mhisani wa wanadamu na rehema kwa ulimwengu wote na kuiondolea heshima Islam.

Lakini hawaelewi na hawajui wanakoelekea. Wakati amri ya Mungu itakapotimia na Inshallah itatimia, watu hawa watateketezwa. Sio wakandamizaji watabakia wala wale wanaosaidia ukandamizaji. Hivyo tunahitaji kuomba na kuomba kwa wingi. Mwenyezi Mungu awakomboe watu kutoka kwenye usingizi waliolalishwa na masheikh na wawe wenye kuelewa ukweli na kumpokea Imam wa zama.

Huzur alisema ataongoza jeneza ghaib baada ya sala ya Ijumaa.

Hotuba ya Bw. Ode - Amir wa Falastin

Kutoka uk. 2

kutimia kwa shani yake yote. Matukio yako mengi yanayoonesha ya kuwa kwa namna gani Mwenyezi Mungu Anawateremshia malaika wenye tabia njema,hata hivyo naeleza tukio moja tu.Siku moja rafiki yangu ambaye ni mshiya alinipigia simu kutoka Irak na kusema kwangu ya kuwa,mimi nilikuwa sijui chochote wala lolote kuhusu Syedna Ahmad as na Jumuiya yake,usiku mmoja kwa kuhuzunika juu ya hali ya mauaji yaliyotokea nchini Iraq,nilipolala, nikamwona kwenye ndoto mtu mmoja alikuwa akitoa hotuba yenye fasaha na balagha katika mkusanyiko mkubwa.Mimi nilifikiri kwamba huyu alikuwa Hadhrat Ali ra.Nilianza kusogea mbele ili nimwambie yaliyonisibu,hapo ndoto ilikwisha na kutoka hotuba yake ubeti mmoja ulibaki kichwani mwangu ambao ulikuwa ubeti wa Kiarabu wa Syedna Ahmad as ambamo ndani yake Huzur alisema ya kwamba sisi tumeiacha dunia hii na kwa kutanguliza jamali ya rafiki yule tukauacha uzuri wa dunia hii.Baadaye mimi nilianza kuutafuta ubeti huo,niliwauliza masheikh wa kishia na kuutafuta sehemu zote lakini haukupatikana.Siku moja nilikuwa nikibadilisha chaneli mbalimbali kwamba ghafla MTA Alarabia iliwaka ambamo ndani yake ubeti huu ulikuwa ukisomwa,wakati ule ule picha ya Syedna Ahmad as ilionekana kwenye kioo cha televisheni ambayo chini yake ilikuwa ikiandikwa, Imam Mahdi na Masihi Aliyeahidiwa,yeye anasema kwamba kwa kuona hayo,mwili wangu ulianza kutetemeka na ilitoka mdomoni mwangu kwa sauti ya juu Allahu Akbar,Allahu Akbar Imam Mahdi Amekwishadhihirika. Alhamdolillah Alhamdolillah Awwalan wa Aakheran.

Tamati

Hutuba hii ilitolewa na Amir wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya Palestina Bwana Muhammad Sharif Odde wakati wa mkutano wa Qadiyan mwaka 2013.

Mfasiri: Sheikh Waseem Ahmad Khan Tabora

Ij'timaa ya Khuddam yaleta Mapinduzi Mapya

Kutoka uk. 1

kujitolea kwa ajili ya Jumuiya basi tutakuwa ni miongoni mwa watu wenye hasara.

Awali, katika hotuba yake ya ufunguzi wa Iijtmaa hiyo, Sadr Khuddamul Ahmadiyya Tanzania, Dkt. Swaleh Kitabu Pazi aliwakumbusha vijana umuhimu wa Ijitmaa na kuwataka kujitahidi kadri ya uwezo wao kuhakikisha wanashiriki kwa ukamilifu katika shughuli mbalimbali zitakazo kwenda samba na Ijtmaa hiyo. Aidha, Sadr Sahib aliwakumbusha khuddam kuishi kwa Amani, Upendo na kuhurumiana kwa kipindi chote watakachokuwa katika ijitmaa na kujiepusha na mambo ambayo yatawaweka mbali na radhi za Mwenyezi Mungu.

Mashindano yaanza rasmi

Mara baada ya mashindano mabalimbali ya kielimu na kimwili yalianza rasmi kwa upande wa Khuddam. Mashindano ya kimwili kama vile mpira wa miguu yalinza majira ya saa kumi na moja jioni kwa kuzikutanisha timu ya Ahmadiyya Sekondari na Jamia.

Atfal wafanya Ufunguzi wa Ijtmaa yao ya Pili mwaka huu.

Mara baada ya ufunguzi wa Ijtmaa kwa pamoja, Sadr Sahib pamoja na Masadr waalikwa, walikwenda kwenye ukumbi wa pili kwa ajili ya kufungua rasmi Ijitmaa ya Pili ya Atfalul Ahmadiyya. Atfal walionesha utulivu na nidhamu ya hali ya juu kwa muda wote wa ufunguzi wakiongozwa na Viongozi pamoja na wasimamizi wao ambao walishirikiana bega kwa bega kuanzia mwanzo mpaka mwisho wa Ijitmaa hiyo.

Mashindano yapamba moto siku ya pili

Siku ya Pili, yaani Jumamosi ya tarehe 21 Juni 2014, mashindano yalizidi kushika kasi ambapo vijana wengi walipata nafasi ya kuonesha vipaji na uwezo wao katika hatua mbalimbali za mashindano hayo. Asubuhi, mashindano ya kimichezo kama vile riadha, kuvuta kamba na mpira wa miguu yalifanyika kwa ushindani wa hali ya juu na kuleta msisimko mkubwa miongoni mwa washiriki na watazamaji kwa ujumla.

Mashindano ya kielimu yaliendelea ambapo kwa upande wa Atfal, wakati shindano la Hifdhil Quran likiendelea, Sadr Sahib wa Uganda alivutiwa na usomaji wa Qur'an wa Atfal kadhaa na kuwaomba warudie kwa ajili yake ambapo nao bila kusita walifanya hivyo kwa mapenzi.

Ijitmaa yafikia kilele

Kadri siku zilivyosonga ndivyo msisimko ulivyozidi kwa washiriki. Siku ya tatu ya mashindano hayo, wageni kutoka nchini Kenya walirejea kwao kuwahi majukumu mbalimbali ya kikazi. Viongozi na washiriki waliwaaga ndugu zao hao kwa mapenzi mapema asubuhi kabla ya kuondoka viwanjani hapo.

Mashindano yaliendelea kabla ya ufungaji rasmi wa Ijitmaa. Masheikh kutoka Jamia Morogoro waliungana na Viongozi wa Khuddam kuendesha mashindano mbalimbali ya kielimu. Wageni kutoka Uganda walipata nafasi ya kushiriki katika mchezo wa mieleka ya mikono (Arm wrestling)na kuoeshaushindani mkubwa japo khuddam kutoka Tanzania aliibuka mshindi.

Amir na Mubashiri Mkuu, Sheikh Tahir Mahmood Choudhry, ndiye aliekuwa mgeni rasmi ambapo katika hotuba yake ya kufunga Ijtmaa hiyo, alisema kuwa ……..

Tukio lililosisimua zaidi

Tukio lililosisimua au kuleta hamasa Zaidi ni lile lililofanywa na ndugu wawili kutoka Kenya ambao si Waahmadiyya. Ndugu haowawili…….ambao ni Waislamu wa madhehebu ya Shia, walipata taarifa wakiwa nchini Kenya juu ya Ijitmaa ya khuddam wa Tanzania siku ya Ijumaa ambayo ilikuwa siku ya Ufunguzi wa Ijitmaa. Siku hiyohiyo walitafuta usafiri na kuanza safari ya kuja nchini wakiwa na shauku ya kuhudhuria Ijitmaa hiyo. Siku ya Jumamosi walifanikiwa kufika katika ukumbi wa Mashindano na kushangazwa na namna ambavyo khuddam walivyofanya mambo mbalimbali kwa umoja, ushirikiano na kwa nidhamu ya hali ya juu.

Vyombo vya habari vyaripoti kuhusu Ijtmaa

Wakati Ijitmaa ikiendelea katika viwanja vya Jalsa Gaal, Kitonga, vyombo mbalimbali vya habari vilitoa taarifa juu ya matukio yaliyokuwa yakiendelea. Kituo cha Televisheni ya Taifa (TBC 1) kupitia kipindi chake cha Jambo asubuhi ya Jumatatu ya tarehe 23 Juni, kilitoa taarifa kuhusu Ijitmaa. Siku iliyofuata, gazeti linalotoka kila siku la Majira pia lilitoa taarifa kwa umma kuhusu Ijitmaa.



MAOMBI

Hadhrat Ameerul Muminuun Khalifatul Masih V (atba) katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 30/5/2014 amewaagiza Wanajumuiya wote duniani kuomba kwa wingi maombi yafuatayo:

1. Sura Al-Faatiha

(بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ۔اَلْحَمْدُلِلّٰهِ رَبِّ الْعَالَمِيْنَ۔اَلرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ۔مٰلِكِ يَوْمِ الدِّيْنِ۔ اِيَّاكَ نَعْبُدُ وَ اِيَّاكَ نَسْتَعِيْنُ۔
اِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيْمَ۔صِرَاطَ الَّذِيْنَ اَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ۔غَيْرِ الْمَغْضُوْبِ عَلَيْهِمْ وَلَاالضَّآلِّيْنَ۔)

“Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu. Sifa zote njema zinamhusu tu Allah Aliye Mola wa walimwengu wote. Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu, Mmiliki wa siku ya malipo. Wewe tu twakuabudu, na Wewe tu twakuomba msaada. Utuongoze njia iliyonyooka, Njia ya wale Uliowaneemesha, ambao hawakughadhibikiwa na ambao hawakupotea.”

2. Durud Sharif - Kumsalia Mtume

(اَللّٰهُمَّ صَلِّ عَلٰى مُحَمَّدٍ وَّعَلٰى اٰلِ مُحَمَّدٍ كَمَا صَلَّيْتَ عَلٰى اِبْرَاهِيْمَ وَعَلٰى اٰلِ اِبْرَاهِيْمَ اِنَّكَ حَمِيْدٌ مَّجِيْدٌ
اَللّٰهُمَّ بَارِكْ عَلٰى مُحَمَّدٍ وَّعَلٰى اٰلِ مُحَمَّدٍ كَمَا بَارَكْتَ عَلٰى اِبْرَاهِيْمَ وَعَلٰى اٰلِ اِبْرَاهِيْمَ اِنَّكَ حَمِيْدٌ مَّجِيْدٌ۔)

“E Allah, msalie Muhammad na wafuasi wa Muhammad kama Ulivyomsalia Ibrahimu na wafuasi wa Ibrahimu. Hakika Wewe ndiwe Uhimidiwaye Utukukaye. E Allah, mbariki Muhammad na wafuasi wa Muhammad kama Ulivyombariki Ibrahimu na wafuasi wa Ibrahimu. Hakika Wewe ndiwe Uhimidiwaye Utukukaye.”

3 - سُبْحَانَ اللّٰهِ وَبِحَمْدِهٖ سُبْحَانَ اللّٰهِ الْعَظِيْمِ اَللّٰهُمَّ صَلِّ عَلٰى مُحَمَّدٍ و اٰلِ مُحَمَّدٍ۔

“Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu na sifa Zake, Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu Mwenye adhama. Ee Mwenyezi Mungu Msalie Muhammad na ahali (watu) wa Muhammad.”

4 - رَبَّنَا لَا تُزِغْ قُلُوْبَنَا بَعْدَ اِذْ هَدَيْتَنَا وَهَبْ لَنَا مِنْ لَّدُنْكَ رَحْمَةً اِنَّكَ اَنْتَ الْوَهَّابُ۔

“Mola wetu, Usiipotoshe mioyo yetu baada ya kutuongoza, na Utupe rehema kutoka Kwako, hakika Wewe ndiwe Mpaji Mkuu. (3:9).”

5 - رَبَّنَا اَفْرِغْ عَلَيْنَا صَبْرًا وَّ ثَبِّتْ اَقْدَامَنَا وَانْصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِيْنَ۔

“Mola wetu, tumiminie subira, na Utuimarishe miguu yetu, na Utusaidie juu ya watu makafiri. (2:251).”

6 - اَللّٰهُمَّ اِنَّا نَجْعَلُكَ فِيْ نُحُوْرِهِمْ وَنَعُوْذُبِكَ مِنْ شُرُوْرِهِمْ۔

“Ee Mwenyezi Mungu tunakuweka wewe mbele ya vifua vyao (yaani uwe kinga yetu dhidi yao) na tunajikinga kwako na shari zao. “

7 - اَسْتَغْفِرُ اللّٰهَ رَبِّيْ مِنْ كُلِّ ذَنْبٍ وَّاَتُوْبُ اِلَيْهِ۔

“Ninamuomba Allah Mola wangu, msamaha wa dhambi zangu zote na ninatubu / naelekea Kwake.”

8 - رَبِّ كُلُّ شَيْءٍ خَادِمُكَ رَبِّ فَاحْفَظْنِيْ وَانْصُرْنِيْ وَارْحَمْنِيْ۔

“Ewe Mola, kila kitu kinakutumikia Wewe, Ee Mola, Utulinde, Utusaidie na Utuhurumie”

9 - رَبَّنَا اغْفِرْلَنَا ذُنُوْبَنَاوَاِسْرَافَنَا فِيْ اَمْرِنَا وَثَبِّتْ اَقْدَامَنَا وَانْصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِيْنَ۔

“Mola wetu, Tughofirie madhambi yetu na kupita kwetu kiasi katika mambo yetu na Uiimarishe miguu yetu na Utusaidie juu ya watu makafiri. (3:148).”

10 - يَارَبِّ فَاسْمَعْ دُعَائِيْ وَمَزِّقْ اَعْدَائَكَ وَ اَعْدَائِيْ وَاَنْجِزْ وَعْدَكَ وَانْصُرْ
عَبْدَكَ وَاَرِنَا اَيَّامَكَ وَشَهِّرْلَنَاحُسَامَكَ وَلَاتَذَرْمِنَ الْكَافِرِيْنَ شَرِيْرًا۔

“Ee Mola, basi Yasikie maombi yangu na Uwasage maadui zako na maadui zangu na Utimize ahadi yako na Umsaidie mtumishi wako na Utuonyeshe siku zako na Ulinoe kwa ajili yetu panga lako na Usimbakishe hata mmoja miongoni mwa makafiri mfanya vitimbi.”

Bustani ya Washairi

MASIHI AMESHAKUJA

1. Kwa jina la Rahmani, naomba kutoa hoja,
   Tokea hapo zamani, tulikuwa tukingoja,
   Manabii wa Zamani, vinywani walimtaja,
   Tayari masihi kaja, mwangojea kitu gani?

2. Mbinguni na ardhini, ishara zimedhihiri,
   Jua na mwezi yakhini, vimepatwa siosiri,
   Vita, njaa na tauni, dunia vimeathiri,
   Tetemeko la bahari, hivi subira ya nini?

3. Isomeni Qur'ani, arobaini na tatu,
   Hamsina nanendani, kuna mfano wa mtu,
   Anokuja duniani, kuwaunganisha watu,
   Katumwa na mola wetu, sasa mashakaya nini?

4. Pimeni huu wakati, mtaziona ishara,
   Kuwepo kwa jamaati, sijambo la masikhara,
   Msipuuze nyakati, mtaivuna hasara,
   Uwingi sio kafara, ukweli hamtafuti?

5. Kumpokea Masihi, sio jambo la khiyari,
   Muislamu sahihi, niyule aliyekiri,
   Masihi kumkebehi, ni aibu ya dhahiri,
   Na sio tija kiburi, ni vipi tuwanasihi!

6. Masihi ni wetu wote, sio wetu peke yetu,
   Mtume wa dini zote, ametumwa kati yetu,
   Atutwae sisi sote, ashindishe dini yetu,
   Eti mwasema siwetu, neema gani mpate?

7. Fikirini kwa makini, msifanye ukaidi,
   Hashuki Isa mbinguni, wala si yamungu jadi,
   Na zamani kumbukeni, eliyasi hakurudi,
   Kwa nabii Ahmadi, ubishi wafaanini?

8) Ameamua Mwenyezi, Ahmad kumleta,
   Iii afanye ulinzi, na bidaa kuzifuta,
   Amri ya mwenyeenzi, haina budi kufata,
   Ishara zake si tata, jamani hamchunguzi?

9. Fungeni arobaini, kwa maombi na kusali,
   Pia sadaka toeni, majibu hayako mbali,
   Hakika mtabaini, huyu Masihi wa kweli,
   Kwa mungu hakuna mbuli, mbona atawajibuni?

10. Someni kwa wayahudi, niwapi walianguka,
    Walifanya ufisadi, talmudi kuandika,
    Yaani kwa makusudi, taurati kuifyeka,
    Wakajipiga mweleka, kipi walicho faidi?

11. Qur' ani mwaiacha, mwongozo wakewajudi,
    Ukwe1imnauficha, mmekuwa mahasidi,
    Achotae kwa pakacha, hawezi kiu kufidi,
    Chemchem twafaidi, nyie vipi mwaikacha?

12. Dunia yetu msitu, ikiza kinene ndani,
    Imam mahdi wetu, ni tunu kwa waumini,
    Hatuwezi ona kitu, ila masihi nimboni,
    Kubali mpokeeni, mwatakashimo la chatu?

13. Vitabu vyake someni, mjipatie elimu,
    Alafu tafakarini, vizuri mtafahamu,
    Nie1imu yenye shani, katu si ya mwanadamu,
    Niuwezo wa karimu, zindukeni hamuoni?

14. Tuseme kwa lugha gani, mpate kutue1ewa,
    Mwajemi wa Qadiani, ahadi tuliopewa,
    Atashuka mnarani, ijumaa kuzaliwa,
    Leo tumetimiziwa, mnabeza kitu gani?

15. Mashekhe na maamuma, wote mnao wajibu,
    Tafakari na kupima, iii mpate majibu,
    Wasomi, wasiosoma, haitakuwa sababu,
    Hamjui mtajibu, hiyo siku ya kiyama?

16. Mwisho ninakhitimisha, na dua kuwaombea,
    Nyoyo zipate bashasha, masihi kumpikea,
    Walio kwene dirisha, wajue pakutokea,
    Amina naitikia, dua nayo mwakanusha?

MWL NAJAT FAKIA SAID
MARUNGU TANGA.

TUACHE

1. Kalamu naikamata, narudia kuandika,
   Uongozi ukipata, usione umefika,
   Na ukawa dikteta, ulimbukeni kushika,
   Tuache kughafilika, duniani tunapita.

2. Kitugani utapata, kama sio kuanguka,
   Hata muda ukipita, anakuona rabbuka,
   Jua shari watafuta, na moto unaukoka,
   Tuache kughafilika, duniani tunapita.

3. Mapungufu watafuta, kwa wenzio hunashaka,
   Kasoro ukizikuta, matangazo kuandika,
   Ya kwako waya fumbata, yenye mbingu kushituka,
   Tuache kughafilika, duniani tunapita.

4. Mola wetu katuita, insi si malaika,
   Banzi lakufurukuta, kwa maneno ukifoka,
   Na umesahau hata, Boriti ulo jivika,
   Tuache kughafilika, duniani tunapita.

5. Kiasi umeipita, kwa kutaka kusifika,
   Uvivu umekumbata, na kupata unataka,
   Matumaini wakata, waja wanahuzunika,
   Tuache kughafilika, duniani tunapita.

6. Unawapeleka puta, hutaki kuajibika,
   Mambo yasipotakata, wafura kukasirika,
   Na maneno unabwata, ya si mema kuropoka,
   Tuache kughafilika, duniani tunapita,

7. Kama wataka kuchota, mto unobubujika,
   Unapaswa kuavuta, na karibu kuaweka,
   Mawazo mkichakata, hapo mtafaidika,
   Tuache kughafilika, duniani tunapita.

8. Kila ulipo kamata, uadilifu kumbuka,
   Usiwe mwenye kusita, kwa kujitoa sadaka,
   Utaondoa matata, na malengo kuyafika,
   Tuache kughafilika, duniani tunapita.

9. Nimefikia nukuta, kalamu chini naweka,
   Sina nia ya kusuta, kwa kila ana husika,
   Vyeo hatukuokota, ni mola ametuvika,
   Tuache kughafilika, duniani tunapita.

MWL. NAJAT FAKIM SAID.
MTITI - TANGA.

1. Mola wetu Subhana, Wewe twakuomba sana
   Tulee sisi vijana, Tufike vyema mwakani

2. Leo hii twaagana, Tangu juzi hadi jana
   Vyema tulitangamana, Kwa huruma na amani

3. Kwa mengi tumeshindana, Nguvu tukaonyeshana
   Na akili kupambana, Kwa mapenzi na hisani

4. Tunawashukuru sana, Khuddamu kuandamana
   Tena tuka ambatana, Kwa utii na makini

5. Twawapongeza mabwana, Walioshirikiana
   Wakawezesha kufana, Ijtimai ya shani

6. Wageni poleni sana, Waganda wenye uungwana
   Wakenya tulo shibana, Mwende salama nyumbani

7. Nanyi nyote hadhirina, Wengi mlojimimina
   Mupewe usalimina, Mrudipo mikoani

8. Tunawashukuru sana, Ansaru na Lajina
   Waliosaidizana, Kutimiza madhumuni

9. Viongozi maulana, Walezi wenye maana
   Nanyi hongerani sana, Kwa kutupa kampani

10. Allahumma ghufir lana, Tusamehe ya Rabbana
    Tumesha sameheana, Tuimarishe rohoni

KUAGANA NI LAZIMA

1. Chozi linanidondoka, mie nawe kuagana
   Kwa miezi na miaka, tabia zililingana
   Sasa wewe kunitoka, la kufanya ndio sina
   Kuagana ni lazima, katika maisha yetu.

2. Si dhahama si baraka, si usiku si mtana
   Kazi kabiri hakika, iliweza tendekana
   Na pale palo pasuka, tuliweza kupashona
   Vipi sasa tutashona, sindano imevunjika?

3. Chaki nilipoishika, maneno niliyanena
   Mengine nikaandika, yaweze kuwa bayana
   Sasa hivi patashika, pumzi zinanibana
   Kusimama natetema, kama mlevi wa tembo.

4. Vitabu nilivisaka, nikafika kila kona
   Iii nijue mipaka, aloiweka Rabuka
   Uwezo umepunguka, si kama ule wa jana
   Macho nayo yamechoka, sisomi bila miwani.

5. Makala niliandika, nazo tungo zenye vina
   Zinazohusu rabuka, na rasuli mwenye jina
   Mwili unatetemeka, siandiki la maana
   Kuna kujaa na kupwa, hayo yetu maumbile

6. Katu sikuadimika, kwa nyumba ya Maulana
   Inyeshe mimi hutoka, kwa furaha zaidana
   Samaki hutotonoka, bahari kwake ni janna
   Na mimi yangu bahari, ilikuwa msikiti

7. Kiwakacho huzimika, kaditamati kunena
   Baadhi nimeyaweka, kusema mengi si sunna
   Machache hueleweka, anapopenda rabana
   Na neno langu la mwisho, sifa zote kwa wahabu.

Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)
Kiwalani - Dar es salaam

Kazema amjibu Bishazo

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma Mwingi wa Ukarimu

Leo namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kunijalia yakini juu ya uwepo wake Alhamdulillah. Na pia namtakia Rehema na amani Mtume Mtukufu s.a.w mbaye ni Rehema kutoka Allah s.w. kwa walimwengu wote.

Kwa kuwa makala yako ni ndefu nami nataka kujibu basi nimeamua kujibu page mbili au tatu zako kwa makala nitakayotoa, kwa kuhofia kwamba itakuwa ndefu sana na watu wakapoteza umakini na kinachoendelea.

Katika mstari wako wa kwanza umemtamkia Rehema na amani kipenzi cha Allah Mtume Muhammad (S.A.W) Alhamdullilah. Lakini nina wasi wasi na jinsi wewe unavyoamini kuwa Mtume Muhammadi ni kipenzi cha Allah, imani yako inanifanya mimi niamini kuwa kuna kipenzi mwingine wa Allah aliye zaidi ya Mtume Muhammadi (S.A.W) kwa kutetea kwako yafuatayo:-

1. Nabii Issa bin Mariam yupo hai mbinguni pamoja na Allah.
2. Hakuwambwa pale msalabani (wenye imani hiyo hapo juu huamini pia hili la pili).
3. Mwenyezi Mungu alivunja kanuni Alizoweka Mwenyewe na kutuambia kamwe hutakuta kawaida Zake zikibadirika.
4. Mwenyezi Mungu katuambia uongo! Mungu apishe mbali, pale Aliposema Mitume wote kabla ya MuhammadiSAWwamekwisha kufa.

Ndugu Bishazo, kama kweli unaamini kuwa Mtume Muhammadi ni kipenzi cha Allah kuliko viumbe vyote Alivyoumba Allah basi angekuwa Muhammadi anyanyuliwe kwa Allah na si Nabiii Issa bin Mariam. Kumbuka, makafiri wa Maka walipomtaka Mtume Muhammad S.A.W apande mbinguni awaletee kitabu wakisome hapo wataamini, Mwenyezi Mungu Alimjibia .....Sema: Mola wangu ni Mtakatifu! Mimi sie ila ni mtu tu, Mtume.

Kwa hiyo Akamwacha tu anaabika na watu wale ila kwa Nabii Issa haraka Akafanya yake aliyoshindwa kwa Nabii Muhammad! Bwana Bishazo huoni ya kwamba Mwenyezi Mungu Anamwamuru Mtume saw aseme " Mola wangu ni Mtakatifu" Hawezi Mwenyezi Mungu Akasema hutakuta kawaida Zake zikibadilika na kumbe huko nyuma Akawa ni Mwenye kubadirika na sasa anashindwa kuifanya hiyo kuwa kawaida. Fahamu ya kwamba kupandisha watu na viwiliwili vyao si kawaida ya Allah S.W na Nabii Issa hakupanda kwa namna udhaniavyo wewe. Kumbuka-Mola wetu ni Mtakatifu.

(2) Hakuwambwa Msalabani, je, kwa kuogopa nini, ataumizwa au atauwawwa? Huku Mtume Muhammad SAW aliachwa kuteseka katika bonde lisilozaa kitu, matezo makubwa ambayo hayawezi hata kidogo kulinganishwa na yake ya msalabani, katika masaa matatu aliyokaa Nabii Issa a.s. Na Mtume Mtukufu s.a.w Aliachwa kupata mateso mengine ya kupigwa mawe na kupigana vita na kung'olewa meno sasa kwa Issa bin Mariam anakimbizwa Mbinguni hai na kiwili wili chake!

(3) Kwa kuwepo hai leo Nabii Issa kwa imani yako basi kumbe si kweli mwenye kupewa umri mrefu hupindishwa katika umbo na harudishwi katika hali dhahili kisha anakuwa hajui yale aliyokuwa anajua, inakuwaje leo Issa bin Mariam aikwepe kawaida hii. Mitume hawakupewa miili isiyokula chakula na wala si wenye kuishi milele. Hivi sasa Issa bin Mariam hali chakula lakini kwa mastaajabu ya bwana Bishazo na imani yake yenye makosa, inatuaminisha, Mwenyezi Mungu Anavunja kawaida hii kwa Nabii Issa na kushindwa kuisimamisha kwa Mtume Mtukufu Muhammad (SAW) Je hauogopi kwamba utampa sifa ya kuwa Mwenyezi Mungu si tu Anavunja kawaida zake bali Anasema uongo, Mungu apishe mbali. Sijui LADHA GANI bwana Bishazo unaipata kuwepo Issa bin Mariam mbinguni hai na Mtume kuwa amezikwa hapa aridhini kama Ladha hiyo haikutiwa na shetani katika mionyo ya watu ambao hawaijali Kuruani wala kuitafakari. Katika ndoto tukufu ya Miraji iliyotokea mwaka wa tano wa Utume, na ambayo imeelezwa katika sura ya AN-NAJM (53:3-19) kwa namna ya kimajazi Mwenyezi Mungu Anajieleza kumshukia Mtume s.a.w. Kwa ujumla niweke aya hizi chache kufafanua ninayoyaeleza hapa

53:(5-12) Siyo haya ila ni ufunuo uliofunuliwa. Amemfundisha Aliye ni Mwenye nguvu sana, Mwenye nguvu kubwa Ambaye kisha akatulia katika kiti chake cha Enzi, Alipokuwa katika upeo wa juu kabisa. Kisha Akakaribia na Akateremka. Ndipo akawa umbali wa pinde mbili au karibu zaidi. Na Akamfunulia Mtumishi Wake Aliyoyafunua. Moyo wa Mtume haukusema uwongo kuhusu uliyoyaona.

Ninachotaka kukueleza hapa ni kwamba Mtume kujiona anapasuliwa kifua na moyo kusafishwa kisha kupaa na Jibril ilikuwa ni katika ndoto tukufu za Mtume, mwili wake haukupaa.

Lakini kubwa ni kwamba katika safari hiyo Nabii Issa a.s alikutwa katika mbingu ya tatu akiwa na Nabii Yahaya. Hapo sasa mzima na mfu walikaa pamoja! Na katika safari Tukufu ya pili Mtume Mtukufu anaonyeshwa kuwasalisha Manabii wote waliopita Nabii Issa a.s alikuwa mmojawapo. Tena mzima wako Bishazo na wafu wanakutana wanaonekana pamoja bila kuwapo tofauti. Huku katika kitabu tunaambiwa wazima na wafu hawakai pamoja.

Nabii Issa a.s amekwisha kufa Bishazo. Mtume asingesema laiti Mussa na Issa wangekuwa hai wasingekuwa na njia ila kunifuata.

Kujumuisha yote niliyoyaeleza, Bishazo naomba ujipime na ujihadhari na sirika za watu hao walivyo kama ielezavyo Kuruani.

6:110. Na huapa kwa Mwenyezi Mungu kwa viapo vyao vyenye nguvu kama ikiwafikia ishara kwa yakini wataiamini. Sema; Hakika ishara ziko kwa Mwenyezi Mungu na ni kitu gani kitawatambulisheni ya kuwa itakapofika hawataamini.

6:113. Na Kama hivyo tukamfanyia kila Nabii adui mashetani katika watu na majini. Baadhi yao wanawafunulia wengine maneno ya kuwadanganya, na kama Mola wako Angalipenda wasingelifanya hayo basi waache na wanyoyatunga.

Ishara ziko nyingi kwa Allah lakini tazama ishara ya kwanza tu itakaposhuka tutakuwa si wenye kuamini na hata hizo nyingine zijazo wengi hawataamini.

6:5. Na haiwafikii ishara yeyote katika ishara za Mola wao ila wanaikengeuka.

Naam watatafuta kufanya uadui na ishara hizo na kujidai wao wanajua zaidi.

6:49. Na hatutumi Mitume ila watoao habari njema na waonyao. Na mwenye kuamini na kufanya wema, basi haitakuwa hofu juu yao, wala hawatahuzunika.

6:50. Na wale wanaozikataa ishara zetu adhabu itawaangukia, kwa sababu waliasi.

Tunaona kwamba Mtume s.a.w anaambiwa mara itaposhuka ishara ya kwanza tu hawataamini bali wataasi. Jilinde bwana Bishazo usije ukaangukia kwa watakaohuzunika bila shaka kitabu hiki kitukufu ni kwa kumuonya aliye hai na kwamba watatumwa Mitume waonyao, amini usiwe miongoni mwa waasi..

Mtume s.a.w alisema katika hadithi yake ya kwamba atakaemkubali Masihi wake basi amemkubali yeye na atakaemwasi Masihi wake atakuwa kamwasi yeye.

Mwisho bwana Bishazo nikutahadharishe kuwa isije ukawa miongoni mwa wanaotakabari katika nchi na ukawa katika kundi la maadui wa Manabii. Fahamu kwamba maadui wa Manabii walijiona wapo sawa sana na watoa damu zao na uhai, kumbe masikini, walikwisha jiingiza kwenye kwapa la shetani (mitandao yakijamii, U-tube presentations nk).

7:147 Nitawaepusha katika ishara zangu wale wanaotakabali katika nchi pasipo haki, na wakiona kila ishara hawataiamini na kama wakiona njia ya mwongozi hawaishiki kuwa njia, lakini wakiona njia ya upotevu wanaishika kuwa njia. Hayo ni kwa sababu walizikadhibisha aya zetu na walikuwa hawazijali

Ndugu mpenzi msomaji wa gazeti hili, nimejibu kwa kirefu sana kuhusu kipengele "kipenzi cha Allah, Mtume Muhammadi (S.A.W). Kwa madhumuni ya kuonyesha ghara tuliyonayo WaAhmadiyya kwa ndugu zetu Waislamu madhehebu mengine kuanimisha ya kuwa Allah(S.W) Ana kipenzi mwingine zaidi ya Muhamadi s.a.w na kwa hakika kuzitoa sifa za Uanadamu wa Nabii Issa na hivyo kumfanya awe si mwanadamu na wala si Malaika. Sheikh mmoja kule Tanga katika mjadala na Mu-Ahamadiyya aliwahi kusema hivyo, kwamba, Yesu si mwanadamu na wala si Malaika na alipobanwa zaidi aliishia kusema ni kiumbe special aliyeumbwa na Mungu na hakukumbuka ya kwamba:-

"Hali ya Issa bin Mariam ni sawa na ya Adamu, Aliwaumba kwa udongo kisha Akawaambia kuwa basi wakawa".

Katika paragraph hiyo Bwana Bishazo akaanza kunizushia mikingamo mimi na Jumuiya yangu. Linalosikitisha zaidi ni pale alipoandika kama ilivyokuwa kawaida ya Wa-Ahmadiyya kuendesha dini kwa propaganda badala ya ukweli halisi. Sasa sijui hii hapa ni kama usemavyo wewe propaganda au ukweli unaokuingia moyoni mwako na watu waliojazwa nuru mioyoni mwao basi watakapomkimbilia Allah na wawe si miongoni na walioepushwa na ishara Zake huelekezwa kwenye njia iliyonyooka njia ya Manabii karibuni.

Katika paragraph yako ya pili page ya kwanza unanilaumu kwa kutumia biblia kama rejeo badala ya kutumia sunna, hadith na kitabu cha Allah sasa kihoja kwako bwana Bishazo hata hujaenda mbali unamnukuu seyyidua Ahmadi a/s ambae yey si sunna, hadithi na wala kitabu cha Allah.

Bwana Bishazo katika mijadala ya kielimu namna hii huwezi kuweka mipaka ya kunukuu maana elimu ni mali ya mwaminio, popote aikutapo aichukue aitumie. Juu ya hayo mwenyezi Mungu ameruhusu tuirejee biblia ingawa ni kweli zimetiwa hitilafu nyingi ndani yake kiasi Mwenyezi Mungu kutaka kuifutilia mbali kama si neno lililotangulia kama vile tutamkuta Mtukufu Mtume wetu katajwa humo na kwa bahati nzuri sana kuna hitilafu chache katika nukuu za Yesu mwenyewe. Nukuu yeyote tunayoitumia lazima ikubaliane katika neno lililosawa baina yetu na wao yaani Kuruani Tukufu. Hoja ya kunukuu Biblia naijibu kwa aya hizi hapa:-

4:137 Enyi mlioamini mwaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na Kitabu Alichoteremsha juu ya Mtume Wake, na Kitabu Alichokiteremsha zamani, na mwenye kumkataa Mwenyezi Mungu na Vitabu vyake na Mitume wake na Siku ya mwisho, basi bila shaka amepotea upotevu wa mbali.

3:94 Kila chakula kilikuwa halali kwa wana wa Israel, isipokuwa kile alichojiharamishia Israel mwenyewe kabla haijateremshwa Torati. Sema leteni Torati na mwisome ikiwa mnasema kweli.

Nimechagua aya hii kwa kuwa hapa Mtume mwenyewe anaamrisha Torati iletwe isomwe bila kuzuiwa na hitilafu zilizomo ndani yake.

IMANI YA KUNYANYULIWA MBINGUNI

Bwana Bishazo kusema kweli haya yote uliyoandika katika ukurasa huu mimi nachoka kabisa. Hujagisia kabisa aya niliyotoa katika makala unayojidai kujibu. Aya ya msingi uliyotakiwa kujibu ni hii hapa.

5: 76 Masihi bin Mariam siye ila ni Mtume tu, bila shaka Mitume wamekwisha fariki kabla yake, na mama yake ni mwanamke mkweli; wote wawili walikuwa wakila chakula. Tazama jinsi tunavyowabainishia aya kisha tazama wanageuzwa wapi?

Endelea uk.9

Mwalimu Nyerere na Waahmadiyya

Na Mahmood Hamsin Mubiru

Inaendelea toka toleo lililopita.

Ikumbukwe ya kwamba si wakati wote marafiki hawa wawili - Kaluta Amri Abedi na Julius K. Nyerere - walikuwa katika upinzani hapo shuleni. Kuna wakati ambapo mmoja alitulia na kuweza kumsikiliza mwenzie. Upo wakati Kaluta Amri Abedi alimueleza Julius Nyerere juu ya kitu alichokipenda sana kuliko vyote nayo ni maisha ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Alimueleza ya kuwa maisha ya mteule huyo wa Mwenyezi Mungu yalikuwa ni kitabu kilicho wazi na mfano uliotukuka kwa binadamu wote. Aliendelea kumueleza ya kwamba maisha yale ni kitabu na kila ukurasa wa maisha umeandikwa katika kitabu hicho na ni muongozi kwa binadamu. Alikuwa yatima, hivyo akajifunza subira na uvumilivu. Alikuwa mfanyabiashara akaonesha uaminifu na uadilifu. Alikuwa kiongozi bila kuwa kiongozi. Maisha yake yalikuwa ya kawaida mno. Kuna siku jiko lake lilikuwa limenuna. Kuna wakati alifunga mawe tumboni mwake kupunguza kasi ya njaa. Alilala chini m ara kwa mara. Alishona viatu vyake. Hakuvaa nguo za kifahari. Kutokana na mavazi hayo wageni waliokwenda kumuona kiongozi wa dola walimsalimu kwa heshima zote Hadhrat Abubakar (ra) wakidhani kuwa ndiye mkuu wa nchi. Alikuwa na huruma na alipenda sana kuwasamehe maadui zake. Bedui mmoja aliyekuwa amefanya mipango ya kumdhuru alipelekwa na Seyidina Umar (ra) mbele yake na kwa m shangao mkubwa kwa upande wa Umar (ra) Mtume Muhammad (saw) alimuuliza; "Je umekwisha kula?" Adui huyu alipewa chakula na baadae alisamehewa.

Masimulizi haya yalimsisimua sana Julius Nyerere na akaonesha kuathirika sana. Maisha ya baadae ya Julius yalionesha athari kubwa ya mazungumzo hayo baina ya marafiki hao wawili.

Julius Nyerere alikuwa mbali sana na mambo ya ufahari, kujitutumua na kujionesha. Mavazi yake yalikuwa ya kawaida na ilifika wakati akaachana kabisa na taishingoni. Chakula chake tunaambiwa kilikuwa cha kawaida. Mikogo haikuwa sehemu ya tabia yake. Siku alipopewa nyumba na wanajeshi alishtuka na kusema ya kwamba; "*Nyumba yote kubwa hii kwani mimi tembo*?" alipunguza mshahara wake. Yeye alikuwa ni katika viongozi wachache wa Afrika waliokuwa wanalipwa mshahara kidogo. Wakati jirani zetu kiongozi alitanguliwa na msururu wa magari na ving'ora. Nyerere akipita usingezania kiongozi wa nchi anapita. Hizo ni sifa ambazo ni muhali kumnyang'anya Kambarage Nyerere. Wiki tatu tu baada ya uhuru alijiuzuru kama Waziri Mkuu na akaenda kuishi na watu ili kujifunza zaidi matatizo yao. Katika miezi hiyo ya kuwa na wananchi aliandika vitabu vifuatavyo vitatu:- *Ujamaa wa Kiafrika, The Second Scramble* na *TANU na Raia.*

Binadamu huathirika na anayoyasikia, kuambiwa au kusoma. Bilkhususi anapokuwa kijana bado. Hoja yetu ni kwamba mazungumzo hayo ambayo tumeyaona hapo juu yalisaidia kwa kiwango fulani kumtengeneza yule ambaye mwandishi mmoja wa Kiingereza alimwita *'Political saint'* – Mwanasiasa mtakatifu.

Hapana shaka Nyerere alikuwa ni binadamu ambaye hakukosa kasoro. Na haya aliyasema yeye mwenyewe na aliwahi kuandika kitabu; 'Tujisahihishej'. Lakini kwa ujumla wa yote alijitahidi katika kuwa karibu na wananchi na ni dhahiri ya kwamba mazungumzo yale na rafiki yake pale shuleni yalitoa mchango mkubwa.

Kutoka shuleni Julius Nyerere na Kaluta Amri Abedi walikutana mara ya pili katika harakati za kupigania uhuru na ujenzi wa taifa jipya. Mwaka 1950 Kaluta Amri Abedi alikuwa Katibu wa Tanganyika African Association (TAA). Habari za Nyerere zilikuwa zinasikika sikika na wale aliokuwa nao Tabora School na wale aliokuwa nao Makerere. Nyerere na Kaluta walikuwa wakitembeleana na Nyerere alipenda sana kumtembelea Sheikh Amri msikiti wa Ahmadiyya Masjid Salaam uliyopo mjini Dar es salaam - Mnazi Mmoja. Hata Kaluta Amri Abedi alipokwenda kusoma Rabwah –Pakistan aliendelea kupata habari za mapambano ya uhuru kutoka kwa mpwa wake Sheikh Saadani Abdul Kandoro na Julius Kambarage Nyerere.

Aliporudi kutoka Pakistani Sheikh Kaluta Amri Abedi alipangiwa Dar es salaam na hapo alifanya kazi nzuri ya TANU kwa kuchapa barua na misaada mingine ambayo chama kilihitaji. Julius Nyerere alipokutana na Sheikh Abdulkarim Sharma huko Mombasa alimuuliza Sheikh mbona umetuacha peke yetu Tanganyika? Sheikh Abdulkarim Sharma alimjibu; "*Nimewaachieni Sheikh Kaluta Amri* Abedi". Ni kweli alikuwa amewaachia Sheikh Kaluta Amri Abedi, kwani mara baada ya kutoa ile khotuba yake maarufu katika umoja wa mataifa Julius Nyerere alimuomba Sheikh Amri aitafsiri kwa Kiswahili na akaitafsiri na kupewa jina la; "*Mwito wa Uhuru*". Na ujumbe wa Umoja wa mataifa ulipoitembelea Tanganyika katika miaka ya 1950, ujumbe



wa wazee wa TANU ulikutana na wawakilishi wa Umoja wa mataifa ili kueleza matatizo ya Watanganyika. Na Julius Nyerere kwa niaba ya TANU alimteua Sheikh Amri afanye kazi ya kuwa mkalimani. Mwishoni mwa mwaka 1957 ulifanyika mkutano wa Waafrika katika mji wa Tunis – Tunisia kwa Rais Habibu Bulghiba na TANU ilituma wajumbe wafuatao:- Oscar Kambona, Nsiro Swai, Rashidi Mfaume Kawawa na Sheikh Kaluta Amri Abedi. Walifanya kazi nzuri ya kuwakilisha TANU na Sheih Amri aliwaeleza hatua zilizokuwa zinachukuliwa katika kukienzi na kukiendeleza mbele Kiswahili. Kutokana na umuhimu wa Kiswahili ambao ulijitokeza katika kutafsiri hotuba yake Mwalimu Nyerere aliona umuhimu mkubwa wa kujifunza lugha ya Kiswahili. Na aligundua katika kule kukaa na wale wazee wa TANU akagundua kwamba Waswahili hupenda kunukuu mashairi mara kwa mara wanapozungumza hivyo nae akaanza kujifunza Kiswahili na Mashairi. Nae Mwalimu anakiri ya kwamba Mwalimu wake wa Kiswahili na mashairi ni Sheikh Kaluta Amri Abedi.

Dr. Ahmad Kiwanuka ambaye amewahi kuwa katibu wa CCM huko Pemba, afisa wa CCM Makao Makuu, Mkuu wa Mkoa wa Arusha na Morogoro, Balozi wa Tanganyika, India, alisema ya kwamba alimsikia yaye mwenyewe Nyerere akisema kwamba Tanganyika ina wataalamu wawili ambao wote wanatoka Kigoma. Mtaalamu wa Kiingereza alisema ni Godwin Tunze na mtaalamu wa Kiswahili alisema ni Sheikh Kaluta Amri Abedi.

Tarehe 18 Oktoba 1961 joto la kisiasa lilipanda. Ukumbi wa Karimjee ulikuwa hautoshi. Wiki sita zilikuwa zimebaki kabla ya Tanganyika haijapata uhuru. Serikali ilikuwa imewasilisha muswada uliotoa haki kwa Watanganyika wote kupata uraia bila kujali dini au rangi ya mtu. Baadhi ya wabunge wa bunge hilo waliopewa lakabu ya wabaguzi weusi, walisema Tanganyika ilikuwa ni nchi ya weusi na hivyo wageni wanaweza kufikiriwa tu kuwa wananchi baada ya miaka 7 ya uchunguzi. Wengine wakiwanyoshea mawaziri wasio weusi walitaka wajiuzulu kutoka baraza hilo la mawaziri la Julius Kambarage Nyerere. Mwingine kwa hasira alisema; 'Hawa wakati ukifika lazima wafunge virago'. "Hatuwezi kutawaliwa na wageni lazima wajiuzuru". Julius Nyerere alisimama ili kutoa msimamo wa TANU na kusema kama muswada huo ungeshindwa alikuwa tayari kabisa kujiuzuru. Huo ulikuwa ushindani mkubwa kati ya Demokrasia na ubaguzi wa rangi. Wabunge wengi walikuwa wamezungumza isipokuwa Sheikh Kaluta Amri Abedi. Wabunge wenzie waliokuwa wamefahamu uwezo wake wa kujenga hoja walimuomba azungumze, na kweli wakati wa sala ya Adhuhuri alifika Masjid Salaam na kuwaomba waliokuwa Msikitini wamsaidie katika maombi ili aweze kufanikiwa kujenga hoja madhubuti, ili kuinusuru nchi kutoka kwenye makucha ya ubaguzi wa rangi.

Sheikh Kaluta Amri Abedi wanaeleza waliokuwepo alilia sana kwenye msala na mchana huo akatoa hotuba ambayo muandishi wa '*The making of Tanganyika*' anaisifu sana kwa vile iligeuza upepo katika bunge. Sheikh Kaluta Amri Abedi kwa kutumia msingi wa mafundisho ya Islam na uwezo wake wa miaka mingi wa kuhubiri, kwanza aliwashukuru wabunge kwa kutoa mawazo yao kwa uwazi bila ya woga, na akasema kwamba huo ulikuwa ukomavu wa kisiasa. Na ni jambo linalojenga utamaduni unaotia mbolea mti wa Demokrasia kukuwa. Akiwaangalia wale ambao walikuwa hawakuunga mkono muswada wa serikali, alisema ya kwamba 'wasio wazawa kupewa miaka saba ili kubaini iwapo ni waaminifu wa nchi hii' alisema jambo hilo halieleweki hata kidogo. Uaminifu alisema Sheikh Amri hauwezi kupimwa kwa rangi, na wala kuisaliti nchi hakutegemei rangi pia. Uaminifu ni jambo lililo moyoni. Ni mtizamo, watu wengi wamechukuliwa mahakamani kwa kesi za uhaini, na hao wote walikuwa wazawa, ndugu zetu wanasemaje kwa hilo? Huwezi kuwa muaminifu kwa sababu tu wewe ni mweusi. Wakati tukipigania uhuru baadhi ya ndugu zetu walikuwa upande wa wakoloni, je hawa hawakuwa weusi? Tuwafanyeje sasa? Tuchukie mfuno na sio watu, bustani yenye maua ya rangi moja haipendezi, inatakiwa bustani yenye rangi nyingi. Tanganyika ni bustani y enye rangi nyingi. Majivunuo hayafai. Waingereza walijivuna utawala wao upo wapi? Warumi wapo wapi? Walikuwa na ufalme mkubwa. Wafalme wa Ki-Mughal wako wapi? Tukumbuke kwamba ukweli siku moja utashinda.

Wakati wote wa hotuba hiyo, bunge lilikuwa kimya na inasemekana kwamba ndege angeweza kutua katika vichwa vya wabunge kutokana na utulivu waliokuwa nao. Julius Kambarage Nyerere alitoka kwenye kona alikokuwa anasikiliza hotuba hiyo alikwenda na kumkumbatia Sheikh Kaluta Amri Abedi. Kura ilipopigwa serikali ilishinda, na maisha ya kisiasa ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere yalikuwa yameokolewa na Sheikh Amri Abedi. Hatujui hatima ya nchi yetu ingekuwaje kama Mwalimu Nyerere angejiuzulu?

Lakini lililokuwa linamuuma sana Nyerere ni yale maumivu kuona katika bunge la nchi yake walikuwepo *wafuasi wa sera ya ubaguzi wa rangi*, uliokuwa

Endelea uk.9

Kazema amjibu Bishazo

Kutoka uk. 7

Ulitakiwa katika makala ile ukokotoe aya hiyo kisha ndani yake upate uhai wa Nabii Issa a.s na kwamba Allah Subuhana Wataallah hapo anatushangaa sisi na si wewe na hiyo mbingu yako anayokaa Nabii Issa mpaka leo!

Tazama basi aya inavyobainishwa (kukokotolewa) na kupata kifo cha Nabii Issa a.s. na wala si uhai wake.

(1) Masihi bin Mariam siye ila ni mtume tu.

Mitume wana sifa zifuatazo:-

- Wanaleta ujumbe wa Allah kwa binadamu au hasa kaumu walizopangiwa.
- Wanakuwa ni binadamu
- Wanakutana na upinzani (wanafadhiliwa kupata upinzani)
- Wanakuwa ni wanaume
- Wanaowa na wanazaa
- Ni wakweli na wanalindwa na dhambi
- Wanakula chakula
- Na wanakufa baada ya kuhitimisha kazi walizotumwa kwa watu wao (nyimati zao)

(2) Bila shaka Mitume wamekwisha fariki kabla yake.

- Ni kawaida kufa Mitume hivyo kufa Nabii Issa kisitushangaze. Issa a.s. amekufa.
- Ikiwa angekuwa hai mpaka sasa kanuni za Allah ambazo hazibadiriki kwa binadamu yeyote zingevunjika na kumpa Allah s.w. sifa ambazo si zake.

(3) Na mama yake ni mwanamke mkweli;

- Mama yake amejumuishwa hapa katika Aya hii kwa kuunganishwa Uanadamu wake na ule wa Issa bin Mariam a.s. na wote walitajwa kuwa Ishara katika Ishara za Allah
-

(4) Wote wawili walikuwa wanakula chakula.

- Kwa kuwa Mitume hawakupewa miili isiyokula chakula na mama yake kuwa mwanadamu nae hali chakula sasa basi wote wako katika hali moja ya umauti
-

(5) Tazama jinsi tunavyowabainishia aya kisha tazama wanageuzwa wapi?

- Akina Bishazo wanaamini Allah s.w, juu ya kuwabainishia yote hayo katika aya, wanaendelea kulazimisha Nabii Issa a.s. yu hai mahali panapoitwa mbinguni, Allah s.w. Anawashangaa
- .

Sasa namna hiyo ilikuwa ufanye kisha ulete maana ya kumshirikisha Allah S.W na Nabii Issa akiwa huko unakoita mbinguni ambako kulishushwa vitu vingi hata chuma na manna na salwa pia na kupandishwa vitu vingi hata siku pia na hata Kuruani. Ndugu yangu siku zote maneno kupandisha na kushusha yanapotumika katika Qur'an huwa tu na maana ya kimajazi na Kitabu chake Allah kinatakiwa KUTAFAKARIWA lau sivyo utajikuta unawashangaza watu wenye yakini pamoja nae Subhana Wataallah.

Usomi wako wakushangaza sana unapoandika maneno ya kishabiki bila kutilia maanani sifa za Mwenyezi Mungu. Naandika haya nikiwa na fadhaa moyoni mwangu, je huyo Issa hai anamsaidia kazi gani Allah s.w huko mbinguni?. Au anamwondolea Allah S.W upweke? Kama Alimuumba mbora wa viumbe Muhammadi Mustafa baadae, Anashindwaje kumuumba hata aliye bora zaidi ya Issa a.s wa Waizrael hapo baadae? Umati huu ulio bora uje ukopeshwe Nabii wa Umati wa Mussa hapo baadae? Ambao wachamungu katika ummati huu lau wasiwe Manabii lakina wanaweza kuwa sawa na Manabii wa wana wa Izraeli kwa jaala zao akiwamo Issa bin Mariam mwenyewe.

Je Bishazo unaamini haya au huamini. Basi tafadhali komaa na acha imani hiyo yako ya kishirikina na hata kidogo sikutegemea itoke kwa msomi kama wewe ambapo logic ni nyenzo kubwa katika utendaji wa uliyoyasomea na sasa acha ushabiki na tumia logic uikokotoe ile aya na ututhibitishie uwepo hai wa Nabii Issa na kwamba Allah s.w. Anatushangaa sisi tusemao kinyume chake, hapo kwa hakika utakuwa unajibu makala yangu.

Makala zijazo nitaendelea kujibu page 3,4 na 5 za Bwana Bishazo.

Wabillahi toufiq
Eng. Kaya S. Kazema
Morogoro.

Mwalimu Nyerere na Waahmadiyya

Kutoka uk. 8

unaendelea Afrika ya Kusini. Nyerere alikuwa anafahamika kama mpinzani mkuu wa ubaguzi wa rangi. Akieleza sera ya Tanganyika ikishapata uhuru Mwalimu Nyerere mwezi Marchi 1961 aliahidi kuwa angejitahidi kuepuka makundi katika Afrika na dunia, kwa ujumla alisisitiza juu ya wazo hilo alisema; "Nia yetu ni kuwa na marafiki wa nchi zote duniani, isipokuwa Afrika ya Kusini". Ni dhahiri Nyerere hakujiweka pembeni kuhusu Afrika ya Kusini. Mawaziri wakuu wa Jumuiyya ya Madola walipokutana mwaka 1961 aliwatumia ujumbe wa kuhusu hisia za nchi changa za Afrika kuhusu Afrika ya Kusini. Ni kwa sababu tuna hamu ya kujiunga na umoja wa Madola ndiyo maana jambo la msingi kwetu ni kuheshimu m isingi y a usawa na haki mbele ya sheria kwa wote. Vitu ambavyo ni vya lazima kwa taifa lolote lenye ustaarabu. Msimamo utakaochukuliwa na mkutano wa viongozi wa Madola utaathiri mustakbali wa umoja huo. Nyerere aliendelea kusema ya kwamba ni matumaini ya nchi changa za Afrika na zile zinazosubiri uhuru wake ya kwamba mtasimama kupigania misingi hiyo ya udugu.

Taarifa hiyo ilipokelewa kwa shangwe na heshima kubwa duniani kote. Waliokuwa hawamjui Nyerere wakamtambua kwamba ni kijana aliyekuwa amesimama kwenye misingi aliyokuwa anaiamini.

Nyerere alifafanua zaidi msimamo wake aliposema tunaamini misingi ya Jumuiyya ya Madola itakuwa imesalitiwa Afrika ya kusini ikikubaliwa tena katika umoja huo. Kwa hiyo tunalazimika kusema kuingia kwa Afrika ya Kusini ni kutoka kwetu kwenye umoja huo. Hivyo sakata la wabunge wa Tanganyika kuzungumzia mambo ya ubaguzi wa rangi tena bungeni lilikuwa ni pigo kubwa kwa julius Nyerere na ushindi ulioletwa na Sheikh Kaluta Amri Abedi ulimpa faraja kubwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwani msimamo wake juu ya ubaguzi wa rangi usingekuwa na maana yoyote wakati nchini mwake ubaguzi wa rangi ulikuwa umejaa tele. Na watu bila shaka wangemuambia kwamba atoe kwanza kibanzi kilichokuwa katika jicho lake kabla ya kutoa boriti zilizokuwa katika macho ya wengine.

Tunaweza kuhisi shukrani kubwa aliyokuwa nayo Mwalimu Nyerere kwa Sheikh Amri Abedi kuwezesha muswada huo kupita licha ya tufani kubwa la kisiasa lililokuwa linatikisa bunge la Tanganyika.

Kwa mara ya pili wanafunzi hawa wawili wa Tabora walikutana tena katika uwanja wa siasa mjini Cairo –Misri, mwaka 1964 mmoja akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na mmoja akiwa ni Waziri wa Utamaduni na Maendeleo ya vijana. Wote wawili walikuwa wanaiwakilisha Tanganyika na Zanzibar na ulikuwa ni mkutano wa pili wa umoja wa nchi za Kiafrika. Kwani wa kwanza ulifanyika mjini Adisababa mwaka 1963. Kwame Nkurumah –Rais wa Ghana aliishambulia sana Tanzania katika mkutano wa piliwa umoja wa nchi za Kiafrika uliofanyika mjini Cairo. Kwame alitoa shutuma nzito dhidi ya Tanzania kwa kusema kuwa Tanzania kilikuwa kichaka cha mabeberu na wakoloni. Na adui mkubwa sana wa Afrika. Kauli hiyo ilimpa kizunguzungu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Aliudhika sana pamoja na ujumbe wote wa Tanzania. Mwalimu Nyerere na Sheikh Kaluta Amri Abedi waliingia chumbani na Mwalimu alikuwa amechukia mno na akamuomba Sheikh Kaluta Amri Abedi aandike jibu. Alikuwa anamfahamu vilivyo sheikh Amri Abedi katika ubingwa wake wa kufutu hoja. Sheikh Kaluta naye alikuwa amesikitishwa sana na hotuba ya Kwame Nkurumah. Lakini bahati nzuri alikuwa na uzoefu wa mashambulio ya aina hiyo. Hivyo hayo hayakuwa mageni kwake. Aliandika jibu na kwa haraka akaichapisha hotuba hiyo kwenye mashine. Mwalimu Nyerere aliisoma na akaiona kwamba ilikuwa ni nzuri sana, isipokuwa ilikuwa kali hivyo akashauri ipunguzwe makali. Kazi hiyo waliifanya pamoja na kilichotoka humo ni hotuba iliyomchanachana Kwame Nkurumah na akabaki kuwa kichekesho mjini Cairo. Kwa kebehi kubwa hotuba hiyo ilimdhihaki Kwame Nkurumah kwa kusema kwamba anataka kunyakuwa sehemu ya nchi jirani kwa kisingizio cha umoja wa Afrika, huo ulikuwa ni uvamizi na wa sio ujengaji wa umoja. Na katika hotuba hiyo pia alisisita ya kwamba ni kichekesho ya kwamba Ghana nchi inayojitia kuwa mstari wa mbele katika mstari wa mbele katika ukombozi wa Afrika ilikuwa haijatoa hata senti tano katika mfuko wa ukombozi wa Afrika. Maneno bila vitendo ndio ilikuwa sifa kubwa Ghana. mwalimuNyerere aliisoma hotuba hiyo kwa hisia na ikawagusa wajumbe wengi.

Hatuna mfano wa mapambano ya kielimu aliyoshiriki Mwalimu Nyerere ambao umefikia umaarufu wa mapambano hayo ya Cairo. Nyerere na Kaluta walipokutana matokeo yake ni hiyo hotuba maarufu ambayo imeacha nyayo zake katika mchanga wa historia ya Afrika.

Ni dhahiri Shaikh Amri Abedi na Nyerere walishughulikia sana ustawishaji wa lugha ya Kiswahili. Mwaka 1963 Julius Nyerere alipotoa tafsiri ya 'Julius Kaisari' ya Sir William Shakespear aliyefanya kazi kubwa ya kumsaidia katika kazi hiyo ya kutafsiri ni Sheikh Amri Abedi kama anavyokiri katika utangulizi huo.

Ushahidi mwingine niliupata kutoka kwa Balozi Jaafar Abdallah Msolomi ambaye amewahi kuwa Balozi wetu nchini Guinea ambaye amesema ya kwamba Sheikh Kaluta Amri Abedi walishirikiana sana na mwalimu Nyerere katika uwanja wa Kiswahili na anasema anakumbuka kwamba lile shairi la Sheikh Amri Abedi 'Ndovu akavwila wima sisimizi akakwama' alikuwa ameliweka ofisini mwake Mwalimu na alipenda sana kulighani.

“Mapenzi kwa Wote bila chuki kwa yeyote”

Kutoka uk. 11

ilisimamisha umoja wa kweli wa Mungu kwa vile baadhi ya watu wa mwanzo walimfanya Ezra kuwa mwana wa Mungu wakati wengine walimfanya Yesu kuwa mwana wa Mungu na wengine waliabudu malaika. Alikuwa ni Mtume (saw) aliyeondoa ufisadi wote na alikuwa ni yeye ndiye aliyeinuliwa na Mungu kusimamisha umoja wa Mungu na kwa rehema za Mungu ulisimamishwa kupitia yeye kwa hakika ni kauli mbiu ..... (Laa ilaaha illallaahu Muhammadur rasuulullah) ambayo tunainadi katika adhma zetu na pale mtu anapoingia katika Islam hutamka ... (Laa ilaaha illallaahu Muhammadur rasuulullah) kwa sababu huo ndio Uislam wa kweli.

Pale mtu anapokuwa dhaifu kiroho ni kwa sababu amepoteza uoni wa (Laa ilaaha illallaahu kwa sababu ikiwa mtu daima atazingatia (Laa ilaaha illallaahu) mtu huyo ataokolewa na madhaifu ya kiroho. Lengo sio kutamka tu ... (Laa ilaaha illallaahu Muhammadur rasuulullah) kama ambavyo watu wengi wafanyavyo, wasemapo uongo huusema huo kwa kusema ..... wakati kutamka ..... kunaleta kwenye mazingatio ukubwa wa Mungu na Adhma yake na sifa zake zote na kama ilivyosemwa awali ukweli wa ..... hubainika tu kupitia Mtume Mtukufu (saw). Usipokuwapo utii kamilifu kwa Mtume Mtukufu (saw) mtu hawezi kuelewa barabara umoja wa Mungu wala hawezi kuelewa maonyesho ya umoja huo kwa mapana ambayo ni Qur’an Tukufu wala ambao hawaelewi umoja wa Mungu kwa kupitia utiifu kwa Mtume Mtukufu (saw) wanabaki wamezama katika shirk ingawaje wawe watu wafahamu.

Achilia mbali wasio Waislam, kundi kubwa la Waislam wamewafanya (P.....) na .....waungu wao. Wakati wa Ahmadiyya wanalaaniwa kwa (Mungu apishe mbali) kufanya ilasi (blasphany) dhidi ya Mtume Mtukufu (saw) na kwa hiyo wameondolewa katika kundi la Islam. Kwa kweli ni hawa watu ndio waliokosa kuelewa daraja la Mtume Mutukufu (saw) na matokeo yake wako mbali na umoja wa Mungu.

Katika zama hizi uelewa halisi wa umoja wa Mungu amepewa Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye amepewao kwa sababu ya utii kamili kwa Mtume Mtukufu (saw). Wale ambao dunia wanawaita makafiri ndio washikiliaji wa kweli wa ngao ya umoja wa Mungu. Ilikuwa ni kwa ajili ya utii wake mkamilifu kwa Mtume Mtukufu (saw) ndio maana Masihi Aliyeahidiwa (as) aligundua kwamba Hadhrat Isa (as) alikuwa amekufa kifo cha kawaida na alikuwa ni ushirikina kudhani yuko hai. Maelfu ya Maulamaa na Mamufti kabla yake walimpa sifa za kiungu Hadhrat Isa (as) kwa mfano kwamba alikuwa hai mbinguni, kwamba alikuwa akifufua wafu na kwamba alikuwa na elimu ya ghaibu. Hata hivyo, kwa msaada wa Masihi Aliyeahidiwa (as) hakuna Ahmadiyya hii leo mtoto au mkubwa atakayeweza kufuata fikra hizi. Hali kadhalika yapo mambo mengi ambayo Masihi Aliyeahidiwa (as) alitufahamisha kupitia utii wake kamili kwa Mtume (saw), kwa kuunyonya mwanga wake na kuondoa ushirikina wetu.

Alikuwa ni Masihi Aliyeahidiwa (as) pekee aliyewaonyesha watu wa zama hizi maonesho ya *Laa ilaaha illallaahu Muhammadur rasuulullah* na hii pekee ndiyo dhati ya Islam ambayo yapaswa kupokelewa na kila mtu ambaye anayo imani kamili juu ya umoja wa Mungu. Yanayobaki ni ufafanuzi ambao ni tofauti kwa watu tofauti, kama ambavyo Mtume Mtukufu (saw) aliwaambia baadhi ya watu kwamba wema mkukbwa ni mtu kuwasaidia wazazi wake, wakati aliwaambia wengine kwamba wema mkubwa ni Jihad katika njia ya Mungu na bado wengine aliwaambia kwamba wema mkubwa ni kusali sala ya Tahajjud. Kwa hivyo akatilia fahamuni mwa kila mmoja maana ya kuondoa udhaifu wao wa msingi lakini hii haikumaanisha kwamba hawakuhitajika kutekeleza maamrisho mengine.

Yapasa ikumbukwe kwamba mafundisho yote ya Qur’an Tukufu ni mazuri sana na yenye manufaa kila moja kama lilivyo, lakini “*Laa ilaaha illallaahu Muhammadur rasuulullah*” linatawala juu ya yote. Hii ndio kauli mbiu ya kweli ambayo yatupasa kuizingatia wakati wote na tunahitaji kutafakari juu ya haja ya umoja wa Mungu na usimamishwaji wake. Umoja wa Mungu haumaanishi tu kwamba mtu asiwe muabudu masanamu au asimshirikishe mtu kuwa hai kama alivyo hai Mwenyezi Mungu au kumshirikisha mtu kuwa sawa na Mungu, bali Umoja wa Mungu una uhusiano na kila kitu katika ulimwengu. Mtume Mtukufu (saw) alikuwa akitamka umoja wa Mungu wakati wa kwenda kulala na wakati wa kutawadha. Kila mtu anapokuwa tegemezi kwenye njia fulani za kidunia hapo anafanya shirk na madai yake ya kuamini Umoja wa Mungu yanabatilika kwa sababu Umoja wa Mungu unalazimisha kwamba mtu amtegemee Mungu pekee. Maana hasa ya Umoja wa Mungu ni kwamba mtu amtazame Mungu Mmoja pekee kwenye kila kitu, kikiwa cha kiroho au cha kidunia. Hakuna shaka kwamba sentensi zote nzuri ni kauli mbiu nzuri, lakini ili kuwa mwaminio halisi katika umoja wa Mungu ni muhimu kwamba kila kitu minghairi ya Mwenyezi Mungu kihafifishwe kwa ajili yake. Kwa hiyo kauli mbiu ya kweli ni; “Laa ilaaha illallaahu Muhammadur rasuulullah” - ambamo mna wema wote na ambayo pia hutoa ufafanuzi wa matatizo yote katika kuelewa Umoja wa Mungu. Mfano mwema uliobarikiwa wa Mtume Mtukufu (saw) uko mbele yetu kuondosha matatizo yoyote na mfano wake uliobarikiwa ulielezwa na Hadhrat Aisha (ra) kuwa ni tafsiri ya Qur’an Tukufu. Sentensi hii inawakilisha kwa kiwango cha juu Umoja wa Mungu, inathibitisha kiwango cha juu cha kutekeleza mafundisho ya Qur’an Tukufu na vile vile inadokeza ufafanuzi wa mafundisho yake kwa hivyo, yeyote anayemuelewa Mtume Mtukufu (saw), anamuelewa Mungu na anaelewa kila kitu kwa sababu shirk ndio mzizi wa kila kitu –ajizi na dhambi.

Kupitia kufungamana na Umoja wa Mungu khulka za hali ya juu, elimu, ustaarabu, siasa na umahiri katika fani nyinginezo huingizwa kwa mtu kwa sababu nuru ya Mungu ni dawa ya kila ugonjwa. Kwa hivyo, kauli mbiu yetu ambayo imechaguliwa na Mungu ni ..... (Laa ilaaha illallaahu Muhammadur rasuulullah) – (Hakuna Apasaye kuabudiwa ila Allah) yaliyobaki ni ufafanuzi ambao waweza kufaa kama ushauri.

Dajjal anaonekana katika nguvu kamili zama hizi na lengo lake ni kutanguliza dunia mbele ya dini, kwa hiyo ni wajibu wetu kuinadi kauli mbiu inayotoa kipaumbele kwa dini mbele ya dunia kumjibu. Hii ndio maana Masihi Aliyeahidiwa (as) ameweka sharti hili kuwa moja wapo ya masharti ya Baiat na inamaanisha kwamba tutashikamana na mafundisho ya dini na tutaonyesha sura nzuri ya Islam kujibu hoja za kila mpinzani kwa kuwa tutafanya yote haya katika kusimamisha “Laa ilaaha illallaahu Muhammadur rasuulullah”

Tumechukua Baiat ya Masihi Aliyeahidiwa (as) katika zama hizi ili kufikia lengo hili.

Ufunuo mmoja wa Masihi Aliyeahidiwa (as) ulisema; ‘Shikilieni vyema Umoja, shikilieni vyema Umoja, enyi wana wa Ajemi’. (Tadhikrah, uk.64, chapa ya 2009). Wana wa Persia – Ajemi haimaanishi familia yake tu, kwa kweli Jamaat yote imelengwa kiroho na hivyo elekezo hili ni kwa Jamaat yote. Imesemwa hapa kwamba shikamaneni na umoja wa Mungu katika nyakati za majaribu ambazo ndio nyakati zote. Ni wajibu wa Jamaat yetu daima kuzingatia kaulimbiu ..... (Laa ilaaha illallaahu Muhammadur rasuulullah).

Leo ushirikina na ukafiri unaenea kwa kasi na hatuwezi kufanikisha maisha yetu katika dunia hii na akhera kwa kujibana katika kauli mbiu moja. Hatuwezi kuacha ibada zetu na sala kwa kujifanya kwetu wasaidizi wa uanadamu. Yeyote afanyaye haya hayumo katika Jamaa ya Masihi Aliyeahidiwa. Twahitaji daima kuzingatia kaulimbiu yetu ya kweli na kusudi letu la kweli ili kwamba tuwe wapokeaji wa baraka za kidunia na kiroho. Mwenyezi Mungu Atuwezeshe sote kuelewa jambo hili.

Hatimaye Huzur alitangaza kwamba ataongoza sala ya jeneza ya Sadiq Akbar Rahman sahib, mtoto wa Faizir Rahman sahib. Alifariki baada ya ugonjwa wa muda mrefu wa kansa tarehe 07 May 2014 katika umri wa miaka 40. Ingawa hakuwa mtumishi wa Jamaat alikuwa siku zote akijitolea sana. Alikuwa na mafungamano thabiti na Ukhalifa na alikuwa na imani kubwa juu ya Mungu na maombi. Alivumilia ugonjwa wake kwa subira kubwa. Mwenyezi Mungu Ampumzishe na kumpatia daraja kubwa peponi. Mwenyezi Mungu Awape subira mama yake na mjane. Ameacha kichanga. Mungu Awe ndio Msaidizi wao na Mlinzi wao

‘Cape of Good Hope’

Kutoka uk. 12

mbalimbali, mabasi makubwa kadhaa ya watalii yalikuwepo, magari madogo ndio usiseme, yalikuwa ni mengi zaidi, kulikuwa na umati mkubwa wa watu. Kuna bango la wastani linalokuleza kuwa hapo ni Cape Point, likikuonyesha ulipo kijiografia kuwa upo kwenye nyuzi {34”21’24” South Latitude na 18”29’51” East Longitude}

Sisi tulikwenda moja kwa moja kusimama kwenye bango hilo na kutimiza ila bishara ya Masih aliyeahidiwa (AS) “I SHALL COURSE THY MESSEGE TO REACH THE CORNERS OF THE EARTH” tulisimama kwa muda huku tukiwa na picha Imam Mahdi na tangazo letu. Wageni wengine nao waliamua kutupiga picha tukiwa na tangazo na picha yetu, kisha tulipoondoka ili kuwapisha na wengine waliotaka kupiga picha za kumbukumbu kwa kufika eneo hilo nao waendelee kupiga. Lakini kama ilivyo ada wengi baada ya hapo wakaanza kutuliza maswali ya kutaka kujua, juu ya ujumbe ule na ile picha ni ya nani. Amir na Mbashiri mkuu alichukua nafasi hiyo kutoa maelezo machache juu ya picha na huo ujumbe. Kisha tukawapatia baadhi ya vitabu na vijarida mbalimbali, walionyesha kuvutiwa kiasi cha wengine kuhoji kama wanaweza kuipata Jumuiya katika nchi zao ili kuweza kujua zaidi. Hivyo kwa hakika ujumbe ulifika, binafsi nilijisikia faraja sana. Najua si kwamba mimi nilikuwa wa kwanza kufika mahali hapo lah, bila shaka wapo wengine waliowahi kufika kabla yetu au kabla yangu. Lakini kwa kila aliyefika basi atakuwa amefika na shani yake, hivyo na mimi alhamdullah nilifika na shani yangu ya kujionea kwa macho tena nikishiriki kutimiza biashara hii tukufu.

Naamini si kusini mwa Africa tu ambako ujumbe umefika, bali kona nyengine nyingi kama si zote ujumbe utakuwa umesha fika, na hivyo kuthibitisha ukweli ya Masih aliyeahidiwa juu ya hili. Ni jukumu la binadamu wenyewe na wenye akili kufikiria, kuamua na kumfuata kwani kwa sasa hakuna njia nyengine ya kimbilio la kweli nje ya silsila hii ya kufungamana na Masih wa zama chini ya Ukhalifa uliopo chini yake.

Baada ya hapo tulipanda kwa miguu juu zaidi ya mlima, juu ya mlima ambako huko kumejengwa mnara wa kuongozea meli, (white house) ukifika hapo juu ndio haswa sasa unaona jinsi hizi bahari kubwa mbili duniani zinavyoungana na pia unaona mwisho wa bara la Africa, kwa maana baada ya hapo hakuna ardhi tena ni mpaka Ametika ya Kusini, Brazil nk. Tulifika huko ingawa kwa tabu kidogo kwani kulikuwa na upepo mwingi mno, mkali haswa, kiasi ambacho tulitakiwa kukaa huko juu kwa dakika chache tu. Kisha tukateremka na kuanza safari ya kurudi. Katika kurudi tulipita sehemu nyengine maarufu inayojulikana kama “CAPE OF GOOD HOPE” Watu wa historia akina mwalimu Mahmoud Khamsin Mubiru na Mwalimu Massamba bila shaka wanaweza kuongea mengi kuhusu “Rasi hii ya Tumaini Jema” ambapo inasemekana msafiri maarufu wa Kireno “Vasco da Gama” baada ya safaari yake ya muda mrefu ya kuzunguka dunia, kupitia baharini, akipotea na bila kujua alikokuwa akienda, hatimae alitokezea sehemu hii, hivyo kupata matumaini mapya

“Mapenzi kwa Wote bila chuki kwa yeyote”

Kutoka uk. 12

ajili ya kupata mapenzi ya MM tu na kusimamisha umoja wa MM. Hatumchukii mtu yeyote, bali tunachukia vitendo vya kishetani na tunawaonea huruma wale wote wanaofuata vitendo hivyo vya kishetani na ni kutokana na huruma yetu hiyo ndipo tunataka kuwaokoa kutoka kwenye vitendo hivi vya kishetani na kuwaokoa dhidi ya adhabu ya MM. Mapenzi yetu kwawanadamu/watuwakidunia hayapo kwa sababu ya faida yoyote ya kidunia, tunachotaka ni hiki tu kuwaondolea chuki zao na hatuhitaji kitu chochote kwao, tunafanya tunayoyafanya kwa ajili ya kutafuta mapenzi ya MM na kusimamisha umoja wake tu. Hivyo tusipaze sauti za kauli mbiu yetu kwa sababu ya kuwavutia wengine bali tufanye hivyo kama njia ya kufikia malengo yetu.

Tunayo bahati kubwa kwamba MA ametuongoza kwenye zama hizi kwenye njia za kupata mapenzi ya Mungu na kufikia njia za kuuonea huruma ubinadamu na ametufunza njia za jinsi ya kuyafikia haya. Amesema:

“Kuna sehemu mbili kubwa za imani, ya kwanza ni kumpenda MM na ya pili ni kuwapenda wanadamu kwa kiasi hiki kwamba mtu azihesabu shida za wengine kama shida zake na ajitahidi kuomba kwa ajili yao.”

Pia amesema: Si jambo zuri wala si jambo lililo sawa kuwatia wengine kwenye shida kwa sababu tu ya tofauti za kiimani.

MA amesema: “Imani yangu ni kutokuwa mgumu hata kwa adui yangu. Ninasema kwa ukweli kabisa, msimhesabu yeyote kuwa ni adui yenu binafsi na jiepusheni sana na tabia ya kukumbatia uadui. ..

Mtu anaweza kufikiria iwapo hakuna chuki kwa yeyote basi tena uadui ni wa nini? Lakini MA ametuambia kwamba tusimhesabu yeyote kuwa adui yetu kati ya wale wanaotufanyia uadui kutokana na tofauti za kidini tu. Tunaweza kuwarekebisha lakini tusiwe na uadui binafsi nao na tujilinde na njia za kudumisha visasi.

Huruma na kuwatakia kheri wanadamu ni aina kubwa ya kumuabudu MM na ni chanzo kikuu cha kupata radhi za MM. Pia MA amsema: “Kuweni wenye kuwatakia mema wanadamu bila kujali imani zao na makabila yao. Walisheni maskini, wapeni uhuru watumwa, na wasaidieni wenye madeni kulipa madeni yao na wasaidieni pia wenye shida zingine na mlifanye hilo kwa sababu ya huruma ya kweli kwa ubindamu.

MA amsema siyapendi maneno ya wale wanaoishia huruma zao kwa watu wa kabila lao / kundi lao tu. Ninawasihi ninyi tena na tena daima msilikunje / msilifanye kuwa dogo duara la huruma zenu. Pia amesema panueni huruma zenu kwa viumbe wa MM kana kwamba ni ndugu zenu wa damu, kama vile mama anavyokunjua mbawa za huruma zake kwa watoto wake. Mtu ambaye anaonesha huruma kama ile ya mama hawezi kamwe kuwa mtu asiye na utu.

Hiki ndicho kipimo cha mapenzi na huruma kwa wengine ambacho kimeamriwa na mM na Mtume wake. Na kimetajwa ndani ya QT. Haya ndiyo mafundisho mazuri ya Islam juu ya mapenzi kwa viumbe wa MM. Je tunaweza kukifikia kiwango hiki mahala popote zaidi ya kutoka kwa mM na kwa yule aliyetumwa kwetu zama hizi kuwa mtumishi wa MT. Bila shaka haiwezekani. Hivyo basi ‘Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote’ lisiwe ndio lengo letu la mwisho bali hiyo ni njia tu ya kufikia mwisho wetu ambao ni kupata mapenzi ya MM

Khalifa Mtukufu akasema kuhusiana na wafanyakazi wa HF kuna wazo kwamba wakitoa huduma zao bila kuzihusisha na imani wanadhani kuwa wanaweza kukubalika zaidi na dunia. Akatoa agizo kwa utawala mkuu wa U.K. walitakiwa kazi zao kuzihusisha na imani na Jamaat ikibidi itajwe wala hakuna tatizo juu ya hilo. Ifahamike kuwa tunahudumia ubinadamu ili kupata radhi ya Mungu. Na tunafanya hivyo kwa sababu hilo ni agizo la Allah la kuwahudumia viumbe. Tuntakiwa kuwa na mfungamano na Mungu na kulinda ibada zetu; kwa maana bila ya hilo hakuna faida ya kuuhudumia ubinadamu kwame. Makao Makuu wakaelewa na Khalifa akawaagiza wafanyakazi na utawala na matawi yote kwa nchi zingine kuwa wengi wao ni Ahmadiyya, hivyo wajenge uhusiano imara na Mungu ili kazi zao zipate baraka za Mungu na waanze kazi zao kwa maombi. Bila ya hili hakuna kazi zetu zitakazo barikiwa ijapokuwa mipango bora ipangwe.

Huzoor (atba) akasema: alikuwa anataka kuongelea jambo hili kwa muda mrefu kwa vile aliona ni suala muhimu kuongelewa. Tukirudi kwenye kauli mbiu; ‘Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote’, Huzoor alitaka kuweka wazi kabisa kwamba hakuna shaka kwamba amali ya kuwatumikia viumbe, huruma kwa viumbe, kuondoa chuki na kueneza upendo ni wema mkubwa, lakini isidhaniwe kwamba kauli mbiu hii ndio kusudi la maisha yetu. Kwa hakika kauli mbiu hii ni nyenzo tu ya kufanikisha lengo, lengo likiwa ni kusudi la maisha yetu. Ni msingi wa ngazi kuelekea kwenye kusudio ambalo kwalo kuja kwa Mtume Mtukufu (saw) kulifanyika na baadae kwa kumtumikia yeye Masihi Aliyeahidiwa (as) alitumwa na Mwenyezi Mungu katika zama hizi ili kufikia kusudio hilo. Na kusudio hilo ni kuingiza uoni wa kweli juu ya umoja wa Mungu na jitihada ya kutekeleza maamrisho yote ya Mungu. Kuufanya mfumo wa maisha uliobarikiwa wa Mtume Mtukufu (saw) kuwa kusudio la mtu na kujaribu kadiri mtu awezavyo kuufikia kwani huo pekee ndio uongozao kwenye kila aina ya khulka njema na wema.

Mjadala ulizuka wakati wa Musleh Mauud (ra) wakati makala zilipochapwa kwenye Al-Fazal (gazeti) au watu maarufu walipotoa maoni yao kuhusu ipi iwe kauli mbiu ya Jamaat. Kauli mbiu iliyotolewa kwa Jamaat na Hazrat Musleh Mauud (ra) au aliyozielekeza fikra za.....kwayo ilikuwa ni yenye kuimarisha Dini zao, kuimarisha imani, na ambayo ilipelekea haki za Mungu kutimizwa hali kadhalika na haki za binadamu. Kulikuwa na watu maarufu wawili kati yao mmoja alipendekeza kauli mbiu yetu iwe ‘Shindaneni basi baina yenu katika mambo mema’ (2:149) wakati wa pili alisema kauli mbiu yetu iwe ‘Mtatanguliza dini mbele ya dunia’. Hadhrat Musleh Mauud (ra) alikubali kwamba kuwepo na kauli mbiu fulani. Taasisi zote duniani zinakuwa na kauli mbiu na kama wako makini na waaminifu katika kufikia kauli mbiu yao, wanafanya juhudi thabiti kufikia kusudio lao ili waweze kutofautishwa na wengine.

Katika dunia visifa hubuniwa kueleza kauli mbiu juu ya maendeleo ya kikhulka, visifa hubuniwa kuelezakauli mbiu juu ya maendeleo ya kielimu na kama haki za binadamu zinalindwa mahala fulani taasisi za kisiasa hufanya uhuru kuwa kauli mbiu yao na hufanya juhudi kufikia lengo hili na kubuni visifa. Kila hali maalum ya sehemu fulani hupelekea kuwepo kwa kauli mbiu maalum. Sababu ya kuwapo kwa kauli mbiu ni kutangaza duniani na wakati huo huo kuweka uzingativu juu ya jambo lile. Kuna maelfu ya malengo mema duniani na ikiwa moja wapo ya hayo limechaguliwa ni dhahiri ni wema kulitumia kama kauli mbiu. Hata hivyo hii haimaanishi kwamba mambo mengine mema hayahitajiki pamoja na hilo. Kwa neno zima kauli mbiu hubuniwa kwa kuzingatia kinachohitajika na kilichopo na kuchagua njia moja bora.

Hadhrat Musleh Mauud (ra) alisema kwamba baadhi ya kauli mbiu zina maungano. Kwa mfano kauli mbiu ‘Mche Mungu’ na ‘Kua kikhulka’ zinategemeana kwa sababu ucha Mungu hauwezekani bila kukuwa kikhulka na mtu asiye na khulka njema hawezi kumcha Mungu. Hali kadhalika kauli mbiu; ‘Nitaitanguliza Dini mbele ya dunia’ na ‘Nitajitahidi kuwa mbele katika mambo mema’ zinafana na zina mahusiano. Hata hivyo kwa kadri kauli mbiu zinavyohusika, wakati fulani baadhi ya watu hujifunga kabisa kwenye kauli mbiu na kuiona ni kila kitu. Mfano watoto wetu na wengineo ambao wamesahau kila kitu kuhusu dini yao lakini ni wapenzi wa kutamka kauli mbiu ‘Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote’ kwa ajili tu ya kujionyesha kwa hakika hii ni kauli mbiu nzuri kuhimizia mafundisho ya Islam kwa ukweli wa moyo lakini sio lengo letu pekee. Huzoor alisema malengo yetu yametapakaa sana. Hali kadhalika heshima kwa viumbe sio kila kitu. Ikiwa kumbuko la Mwenyezi Mungu linakosekana katika mioyo hapo kunakuwa hakuna manufaa.

Hadhrat Musleh Mauud (ra) aliandika kwamba aliposoma makala ya mapendekezo ya kauli mbiu alikumbushwa simulizi ya Myahudi ambaye alimwambia Hadhrat Umar (ra) katika maongezi kwamba alijisikia wivu mkubwa kwa Waislam. Hadhrat Umar (ra) aliuliza nini kilisababisha wivu huo. Yule Myahudi alijibu akasema, wivu ulikuwa kwa sababu Islam ilikuwa na sifa ya pekee kwa vile hakukuwa na chochote ulimwenguni ambacho hakikuwekwa katika amri za Islam, na ambacho hakikuwekwa katika Qur’an Tukufu. Ni kila kitu kutoka kwenye mambo ya binafsi mpaka kwenye masuala ya kimataifa na ufumbuzi wake. Ni hili ndilo linaloleta wivu.

Ikiwa jambo hili litaangaliwa, ni dhahiri kwamba katika Islam si sahihi kupangwa jambo moja lolote kuwa kauli mbiu. Bila shaka ‘.....shindana basi baina yenu katika mambo mema’ (2:149) ni kauli mbiu nzuri na vilevile ‘Nitaitanguliza dini mbele ya dunia’ pia ni nzuri, inatajwa pia katika Qur’an Tukufu kuwa; ‘lakini ninyi mnapenda maisha ya dunia hii, wakati akhera ni bora na ya kudumu zaidi’ (87:17-18) aya hizi kwa kawaida husomwa katika sala ya Ijumaa na kuna mafundisho mengine yasiyo idadi katika Qur’an Tukufu. Hatuna fundisho katika Qur’an Tukufu ambalo haliwezi kutungwa kuwa kauli mbiu; lolote ambalo mtu atalitazama moyo wake utavutika kwalo. Baada ya utangulizi huu, Hadhrat Musleh Mauud (ra) alisema tunajifunza kutoka katika Qur’an Tukufu kwamba wakati wa kufika kwa Mtume Mtukufu (saw) ulikuwa ni udhihirisho wa aya ya Qur’an ‘Ufisadi umedhihiri bara na baharini .....’ (30:42). Kila aina ya ufisadi ulikuwapo wakati huo. Masihi Aliyeahidiwa (as) alikuwa ni (Kivuli / taswira) ya Mtume Mtukufu (saw), kwa hiyo wakati huu pia ni ..... ya wakati wa Mtume Mtukufu (saw). Na tunaona kwamba kila aina ya uharibifu imefikia kilele chake katika wakati huu. Kwa hivyo leo dini inahitajika, kila aina ya khulka njema inahitajika na pia mazuri ya kidunia na maendeleo yanahitajika wakati imani imeondoka kwenye mioyo ya watu ndivyo hivyo hivyo khulka njema zimetoweka na maendeleo ya kweli ya dini yamekoma. Kwa sababu kinachojulikana kuwa ni maendeleo siku hizi kwa kweli ni maonyesho ya ubinafsi, iwe katika ngazi ya mtu binafsi au ya kimataifa. Maendeleo sasa maana yake ni maslahi binafsi tu, hayawezi kuitwa maendeleo kwa ulimwengu kwa sababu ni kundi fulani tu la dunia ndilo linalofaidika kutokana nayo wakati kundi jingine likiwa linakandamizwa. Kwa namna moja au nyingine kundi fulani la dunia linakandamizwa na hakuna maendeleo kwao na wale wanaoendelea wana maslahi binafsi ambayo wanayaita maendeleo.

Kusema kwamba aya hii au ile ya Qur’an Tukufu zifanywe kuwa kauli mbiu na zingine zisiwe ni kukosea. Kila aya ya Qur’an Tukufu yapaswa kuwa kauli mbiu yetu, kama ambavyo kwa hakika ndivyo hivyo, kauli mbiu yetu ni Qur’an Tukufu yote, hata hivyo, ikiwa kauli mbiu nyingine inahitajika, Hadhrat Musleh Mauud (ra) alisema Mwenyezi Mungu Amechagua kupitia kwa Mtume Mtukufu (saw) na ni hii; “***Laa ilaaha illallaahu Muhammadur rasuulullah***” - (Hakuna Apasaye kuabudiwa ila Allah na Muhammad ni Mtume wake). Hii ndio dhati ya Qur’an Tukufu yote na ukweli ni kwamba mafundisho yote na malengo yote makuu yapatikanayo kwa umoja wa Mungu yamo katika kauli mbiu hii. Hali kadhalika mahusiano baina ya watu na kati ya mtu na Mungu vile vile yamo chini ya umoja wa Mungu na umoja wa Mungu hauwezi kuwekwa bayana bila msaada wa Mtume Mtukufu (saw) na hii ndio sababu ..... (Laa ilaaha illallaahu) imefuatiliwa na (Muhammadur rasuulullah). Yule apasaye kuabudiwa kwa maneno mengine Mwenyezi Mungu Anaweza tu kugundulika kwa msaada wa Mtume Mutukufu (saw). Yaani yeye pekee ndiyo njia ambayo kwayo Mungu wa kweli anaweza kuonekana na pale msaada unapotafutwa kufika kwa Mtume Mtukufu (saw) hapo mtu huliona somo la (Laa ilaaha illallaahu) waziwazi kila mahala (katika Qur’an Tukufu). Kutoka sura Al-Faatiha mpaka sura An-Nasi. Ilikuwa kwa hakika ni dhati iliyobarikiwa ya Mtume Mtukufu (saw) ambayo

Endelea uk. 10

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Jamad I/Jamad II 1435 AH | April 2014 | Shahadat 1393 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abdullah bin Umarr.a.yakwambaMjumbewaAllahs.a.w. alisema: Mbora miongoni mwa marafiki ni yule aliye mbora wao kwa mwenzake. Na jirani bora mbele ya Allah ndiye anayemtendea vizuri jirani yake. (*Tirmidhi*)

Khalifa Mtukufu aeleza Falsafa ya: "Mapenzi kwa Wote bila chuki kwa yeyote"

Mara kadhaa tunaiweka kauli mbiu yetu ya Love for all hatred for none = Mapenzi kwa wote chuki si kwa yeyote mbele ya wengine. Tunafanya hivyo ili kuondoa auelewa mbaya kwamba Ahmadiyya Jamaat na wafuasi wake wana chuki au nia mbaya dhidi ya wengine na kwamba eti tunajihesabu sisi kuwa bora kuliko wengine. Pia tunaitumia kauli mbiu hii ili kuweka bayana mbele ya dunia kwamba Islam inafundisha upendo, amani na udugu na kwamba sio sahihi kuihusisha imani ya Islam na ukatili na uovu. Pia tunaitumia kauli mbiu hii kuonesha kwamba tunapenda kuishi pamoja na wengine kwa kuvunjilia mbali kuta zote za chuki. Tunapouhudumia ubinadamu kwa njia yoyote ile au tunapofikisha ujumbe wa Islam kwa wengine (tabligh) tunafanya hivyo kwa sababu tunayo mapenzi kwa kila mtu duniani na tunatamani tuondoa chuki katika moyo wa kila mtu na mahala pake tupande mbegu ya upendo. Tunafanya hivyo kwa sababu hiki ndicho ambacho bwana wetu na kiongozi wetu MT ametufunza. Tumeshuhudia ni vipi alivyohuzunika kutokana na huruma yake kwa wanadamu wakati wa sala zake za usiku akimwabudu Mola wake. Kwa hakika alihuzunika na kulia kwenye sujuda zake mbele ya MM kwa kiwango ambacho MM ameiweka kuwa kumbukumbu ndani ya QT ili iwe kama ushahidi wa wale ambao hawana ubaya na chuki ndani ya nyoyo zao na itadumu hadi siku ya mwisho. Hii imehifadhiwa ndani ya QT ili kwamba wale ambao ilikuwa wake walete upinzani dhidi ya MT katika zama zijazo wapate kutafakari kabla hawajaleta upinzai wao na wale ambao watajinasibisha na Islam wapate kujaribu na kufuata mfano wake mwema. Kwa hakika imesemwa ndani ya QT:

Basi huenda utajiangamiza nafsi yako kwa kusikitikia hali yao ikiwa hawaiamini hadithi hii. (18:7).

Basi ni kipi walikuwa wakikifanya watu wa wakati huo ambacho kilimhuzunisha sana MT. Ni hiki tu kwamba hawakukubali kuachana na kumshirikisha MM, hawakuachana na imani ya kumfanya mtu kuwa mwana wa Mungu. Shirki / kumshirikisha MM ni kosa ambalo MM amelitaja kuwa halisamehe. Ni mapenzi na huruma kwa kila binadamu, hata kwa washirikina ndiyo yanayomfanya mtu afanye juhudi maalum ili kuwaweka kwenye njia iliyonyooka ikiwa ni pamoja na kuwaombea. Ikiwa Waahmadiyya wanao uelewa wa kweli juu ya 'love for all hatred for none', basi wajaribu kila njia na wajitahidi kujifunza njia za mapenzi kutoka kwa bwana wetu na mkarimu wetu MT, na hicho kinatakiwa kiwe ndio kipimo cha kupimia uelewa wetu juu ya Umoja wa MM.

Mfano wa hili ni pale watu wa wakati wa MT walipochupa mipaka yote katika ukatili wao dhidi yake, badala ya kuomba dhidi yao, yeye aliinua mikono wake kumuomba Mungu ili awaongoe. Wakati makabila mengine yalipomtesa yeye aliyaombea kwa mM 'Ee Mola wangu waongoze watu wa kabila linalofanya hivi. Mapenzi yake na huruma yake kwa wanadamu haikuwa kwa ajili yake. Huruma yake ya kuutetemesha moyo ilikuwa ni kwa ajili ya MM tu ili kuiokoa dunia dhidi ya maangamizi. Leo kuna maelefu ya miungu wa bandia (masanamu) inayoabudiwa na sehemu kubwa ya wanadamu hata hawaamini kuwepo kwa Mungu na hivyo basi kuna haja kubwa ya kuiga njia alizotuonyesha MT ili tuweze kuusimamisha ufalme wa MM na umoja (tauhiid) wake duniani.

Tusijidhani wabora kwa sababu tu ya kupaza sauti za kauli mbiu ambayo inaivutia dunia na kusifiwa sehemu mbalimbali. Ni lazima tukumbuke kwamba kauli mbiu hii ni njia moja tu ya kufikia lengo letu kuu tulilo umbwa kwalo. Kazi zetu za ubinadamu, kukuza kwetu njia za kuboresha upendo na kupinga kwetu chuki na kuichukia kwetu chuki ni kwa

Endelea uk. 11

Ujumbe wa Ahmadiyya wafika hadi 'Cape of Good Hope' -

Na Mwandishi wetu
Africa Kusini.

"Nitafiksha ujumbe wako katika kona zote za Dunia" haya ni maneno maarufu katika Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiya duniani kote. Yanaweza kuwa katika aina tofauti za maandishi sawa na lugha ya jamii husika lakini mwisho wake ujumbe utabakia kuwa ni ule ule wa kimsingi. Ni maneno aliyoambiwa Muanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Wasilam wa Ahmadiyya duniani Hazrat Mirza Ghulam Ahamad (as) wa Qadiani zaidi ya miaka 100 iliyopita. Wakati huo alipopewa ujumbe huu wengi wa wapinzani wake waliona ni kama ndoto za mchana haswa ukizingatia hali ya kijiji chenyewe,(Qadian) wakati huo, hali za mawasiliano, miundo mbinu na nk, kwa hakika isingekuwa rahisi hata kidogo kusema kuwa ujumbe huo aliopewa na Mwenyezi Mungu ungefika kwenye hizo kona za dunia. Isipokuwa ni kwa wale tu waliokuwa na yakini ya kweli kwa Muumba na kuamini kuwa hakika kwa Mwwnyezi Mungu hakuna kubwa lisilo wezekana.

Katika makala hii lengo langu haswa ni kutoa ushuhuda japo kidogo tu katika kile ambacho mimi mwenyewe nimekishuhudia. Ni habari rahisi ya jinsi leo hii dunia inavyoshuhudia kutapakaa kwa kiasi kikubwa kwa ujumbe huo, mimi nitazungumzia kwa ufupi tu tulivyoweza kuufikisha ujumbe huo kwenye ncha ya mwisho ya bara la Africa. (Cape Point) katika Jamhuri ya Africa Kusini.



Ilkuwa ni asubuhi na mapema, tarehe 1/12/2013 mara baada ya kumaliza swala ya Alfajiri, ndio tulipoanza kujiandaa kwa safari ya kwenda kutembea kwenye ncha ya mwishoni kabisa mwa bara ya Africa. Safari yetu ilianza kutoka sehemu tunayoishi (Boston) mpaka makao makuu ya Jumuiya huku Africa ya kusini, sehemu inayojulikana kama Athlone. Hapo msikitini tuliungana na Amir na Mbashiri mkuu wa Jamhuri ya Africa Kusini Sheikh Zahir Ahmad na familia yake tayari kwa safari ya kuelekea Cape Point. Safari nzima ilikuwa na wastan wa kilometa 60 mpaka 70 kwenda tu na umbali huo huo kwa kurudi.

Tulianza safari yetu tukiwa na magari mawili tunafuata, tulisafiri kwa umbali wa takriban kilometa 15 hivi, tukafika sehemu maarufu inayoitwa "Camas Bay", hapo ni sehemu maarufu kwani kuna uwanda wa pwani mzuri mno wa pwani wa bahari ya atlantic. Makumi kwa mamia ya watu hependa kwenda eneo ili kuburudika na upepo mzuri kiutoka baharini. Ingawa wenyeji niliongea nao, wengi walisema kuwa, kwa kawaida upepo hapo huwa mkali sawa na asili ya bahari yenyewe ya Atlantic kuwa na mawimbi makubwa mara nyingi. Lakini jambo moja lililonishangaza kidogo ni kuwa, kwa kawaida hii bahari ina papa na samaki wakubwa wengi, hivyo basi baadhi ya wakati husababisha hatari kwa waogeleaji, lakini katika eneo hili hali ni tofauti mno. Pindi inapoonekana kuna hatari yeyote ya wanyama bahari, basi kuna ishara nyingi hutolewa za tahadhari ikiwa ni pamoja na kupigwa kwa kengele za sauti kali mno, ving'ora nk na watu walioko bahari kutakiwa kutoka humo mara moja. Kwa hakika ni jambo zuri mno, maana hii inaonyesha pia maendeleo makubwa ya teknologia. Hatukukaa sana hapo, tukaendelea na safari.

Tulifika katika mji mwengine maarufu wa unaojulikana kama "Simons Town" huu ni mji mdogo tu, lakini una shani yake, kwanza ni mzuri na msafiri, una bandari nzuri ingawa si kubwa sana, mji wenyewe haswa umejengwa juu ya milima ukiangalia bandari au bahari. Inasemekana kwa asili mji huu ulikuwa ukiitwa Simon's Vlek badala ya "Simon van der Stel" ambae alikuwa ni Gavana wa Kidachi wa Rasi ya hii ya kikoloni baina ya mwaka 1677 na 1699. Gavana huyu ndie ambae katika miaka ya 1687 alifanya utafiti na kutembelea eneo hili la pwani, kisha kulielezea kuwa ni eneo zuri na salama wakati wa majira ya kiangazi (Joto) ambayo huwa ni mwezi wa kuanzia na Novemba mpka kwenye mwezi wa March kwa majira ya Cape Town. Kwa sasa pia panajulika kama ni nyumbani kwa jeshi la wanamaji la Africa ya Kusini. (Navy) Pana historia nzuri, ni pazuri, mji umejengwa juu ya milima na chini ni bahari, si lengo langu kuuzungumzia mji huu lakini, tulipita hapo.

Tuliendelea sasa na safari yetu ya msingi, huku tukisimama sehemu mbali mbali njiani, kwa malengo mengi, lakini ikiwa ni pamoja na kuangalia mandhari za maeneo, kuchukua picha nk, kitu kimoja kinachovutia mno au sana katika maeneo haya ni muunganiko wa bahari mbili kubwa, tena moja ikiwa na maji ya moto na nyengine ikiwa na maji baridi. Bahari ya Hindi na bahari ya Atlantic. Ukiwa huku kusini, unaziona zote jinsi zinavyoingiliana. Lakini pia wengi wa watu wa nchi za Africa ya mashariki, tumezoea kuona kuwa bahari huwa pwani, ukiangalia maeneo mengi ya nchi, hususan nchini Tanzania, bahari imepita pwani, maeneo ambayo ni tambarare yasiyokuwa na milima mingi, Tanga, Mtwara, Lindi, Zanzibar nk Lakini huku ni tofauti kabisa na hali hiyo. Huku bahari iko katikati ya milima mizito, milima haswa yenye hadhi ya kuitwa hivyo, mpaka nikafikia kuwaza kuwa, ohh kumbe bara za Africa limeanza kwa milima? Lakini ndio ilivyo huku kusini na mwisho wa bara la letu, sijui kwenye mabara mengine kukoje.

Naam hatimae tulifika kwenye gate ambalo, ukisha lipia na kuruhusiwa kuingia, basi ndio sasa unakwenda huko kwenye ncha kama si mwisho wa bara hili. Kutoka kwenye gate mpaka huko mwishoni ni wastan wa kama kilometa 7-10 hivi, sehemu iliyo na milima na maeneo machache yaliyo tambarare. Hatimae tulifika, "CAPE POINT" ohhh ni sehemu nzuri na iliyojengwa kwa wastani, pakiwa na migahawa na maduka kadhaa ya kuuza haswa vitu vya kitalii. Tulikuta watu wengi kutoka mataifa

Endelea uk. 10